JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2023

# KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE (CSEE) 2023

# 021 KISWAHILI

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2024**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


DIBAJI ............................................................iv

1.0 UTANGULIZI ......................................................1

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI .......................................2

2.1 SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA NA KUOANISHA......... 2

2.1.1 Swali la 1: Kuchagua ..............................................2

2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha ............................................11

2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI ............................. 15

2.2.1 Swali la 3: Tabia za Vitenzi .....................................15

2.2.2 Swali la 4: Uambishaji ...........................................19

2.2.3 Swali la 5: Utata katika Mawasiliano ...........................22

2.2.4 Swali la 6: Fasihi Simulizi .......................................26

2.2.5 Swali la 7: Uandishi wa Insha ..................................32

2.2.6 Swali la 8: Ufahamu ...............................................37

2.3 SEHEMU C: MASWALI YA MAJIBU MAREFU............................ 44

2.3.1 Swali la 9: Uhakiki wa Ushairi ..................................44

2.3.2 Swali la 10: Uhakiki wa Riwaya ................................51

2.3.1 Swali la 11: Uhakiki wa Tamthiliya ............................57

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KATIKA MADA .................63

4.0 HITIMISHO ...........................................................64

5.0 MAPENDEKEZO ....................................................65

KIAMBATISHO PEKEE: UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MWAKA 2023 ..............................................66

## DIBAJI

Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Nne Mwaka 2023 imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakuza mitaala, na wadau mbalimbali wa elimu kuhusu matokeo ya watahiniwa katika somo la Kiswahili kwa ujumla.

Taarifa hii inatoa tathmini ya mwisho inayolenga kuonesha mafanikio ya mfumo wa elimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa watahiniwa wa Kidato cha Nne. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani huu unalenga kubainisha maarifa ambayo mfumo wa elimu uliweza au haukuweza kuwapa watahiniwa katika somo la Kiswahili kwa kiwango cha sekondari, Kidato cha Kwanza hadi cha Nne.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii unalenga kuonesha sababu za watahiniwa kufaulu kwa kiwango kizuri, cha wastani au kibaya katika mada mbalimbali zilizotahiniwa. Ripoti hii inabainisha baadhi ya sababu zilizofanya watahiniwa kujibu vizuri, ambazo ni kuwa na umahiri mkubwa wa mada na uzingatiaji mkubwa wa matakwa ya maswali. Kwa upande wa watahiniwa kuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu, sababu zilizobainika ni kutoa majibu yasiyojitosheza; na sababu zilizofanya watahiniwa wachache kupata alama hafifu katika majibu yao ni kutoelewa matakwa ya swali, uelewa mdogo wa mada zilizopimwa, na uwezo mdogo wa kuelezea kwa ufasaha dhana mbalimbali zinazohusiana na somo la Kiswahili kwa ujumla.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa, mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau wote wa elimu kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, hatimaye kuondoa changamoto zilizobainishwa katika taarifa hii. Pia, Baraza linaamini kuwa, mapendekezo yaliyotolewa mwishoni mwa taarifa hii, yakizingatiwa ipasavyo, kiwango cha ufaulu katika somo hili kitapanda na kuwa bora zaidi katika mitihani yake ijayo.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki katika mchakato wa uandishi wa taarifa hii.

Dkt. Said Ally Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua viwango vya ufaulu wa watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2023 kwa somo la Kiswahili. Mtihani ulikuwa na jumla ya maswali 11 yaliyogawanywa katika Sehemu A, B na C kutoka katika mada za *Ufahamu, Aina za Maneno, Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali*, *Uundaji wa Maneno, Maendeleo ya Kiswahili, Uandishi wa Insha za Hoja*, na *Fasihi*. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika Sehemu A na B, na maswali matatu (3) kutoka Sehemu C.

Viwango vya ufaulu wa watahiniwa vimepangwa katika madaraja mbalimbali ya ufaulu, ambapo madaraja A hadi D yametumika kuwakilisha asilimia ya ufaulu wa watahiniwa waliopata alama 30 na zaidi. Daraja F limetumika kuwakilisha asilimia ya ufaulu wa watahiniwa walioshindwa mtihani yaani waliopata alama chini ya 30. Jedwali Na. 1 linaonesha ulinganifu wa ufaulu wa watahiniwa kwa kila daraja kwa miaka 2023 na 2022.

**Jedwali Na. 1: Ufaulu wa Watahiniwa kwa kila Daraja kwa CSEE 2023 na 2022**

| **Mwaka** | **Waliofanya mtihani** | **Waliofaulu** (%) | **Gredi za Ufaulu** (%) | | | | **Walioshindwa** (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **A** | **B** | **C** | **D** | **F** |
| 2023 | 529,437 | 96.80 | 4.24 | 14.57 | 55.34 | 22.34 | 3.19 |
| 2022 | 522,082 | 95.58 | 3.53 | 13.74 | 56.34 | 21.67 | 4.41 |

Takwimu katika Jedwali Na. 1 zinaonesha kuwa asilimia ya ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2023 imeongezeka katika madaraja A, B na D kwa asilimia 0.71, 0.82 na 0.67 mtawalia. Hata hivyo, ufaulu ulipungua katika madaraja C na F kwa asilimia 1 na 1.22 mtawalia. Hata hivyo, kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2023 ni cha juu ikilinganishwa na mwaka 2022 kwani watahiniwa waliopata alama za daraja la juu waliongezeka zaidi kuliko waliopata daraja la chini la ufaulu.

Ripoti hii inawasilisha uchambuzi uliofanyika ili kubainisha jinsi maswali yalivyojibiwa, jinsi maswali yalivyopaswa kujibiwa, na changamoto zilizojitokeza wakati wa kujibu maswali. Wakati wa uchambuzi, viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni *vizuri*, *wastani* na *hafifu* vilizingatiwa. Kiwango kizuri cha ufaulu ni

alama 65 hadi 100, kiwango cha wastani ni alama 30 hadi 64, na kiwango hafifu ni alama 0 hadi 29. Chati na majedwali yametumika kuwasilisha kwa kifupi viwango vya ufaulu. Katika kila chati, rangi *nyekundu* inawakilisha ufaulu hafifu, rangi ya *manjano* inawakilisha ufaulu wa wastani, na rangi ya *kijani* inawakilisha ufaulu mzuri. Sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatishwa katika kila swali ili kuthibitisha maelezo ya uchambuzi.

Kwa ujumla, uchambuzi huu unalenga kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa walimu, wanafunzi, na wadau wengine wa elimu. Pia, utasaidia kuweka mikakati ya kutatua changamoto zilizojitokeza katika mtihani huu na kuinua kiwango cha ufaulu katika mitihani ijayo.

## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI

Sehemu hii inachambua kwa kina majibu ya kila swali yaliyotolewa na watahiniwa kwa kuonesha maswali yaliyokuwa na ufaulu mzuri, ufaulu wa wastani, na ufaulu hafifu. Aidha, sababu za ufaulu wa watahiniwa katika makundi hayo zimeelezwa bayana kwa kila swali.

### 2.1 SEHEMU A: MASWALI YA KUCHAGUA NA KUOANISHA


Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (2) yenye jumla ya alama kumi na sita (16), ambapo swali la kwanza (1) lilikuwa la kuchagua likiwa na vipengele kumi (10) vyenye alama kumi 10; na swali la pili (2) lilikuwa la kuoanisha maana na dhana katika orodha A na B na lilikuwa na alama sita (6).

#### 2.1.1 Swali la 1: Kuchagua

Swali hili lililenga kupima uelewa wa dhana mbalimbali zinazohusu mada za *Fasihi Simulizi, Uandishi wa Insha, Kuongeza Msamiati wa Kiswahili, Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali, Uundaji wa maneno*, na *Maendeleo ya Kiswahili*. Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kutoka katika machaguo matano (A - E) kwa kila kipengele.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 529,437 sawa na asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Hili ni moja ya maswali yaliyojibiwa vizuri, ambapo watahiniwa 342,867 sawa na asilimia 64.76

walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kiasilimia.





**Chati Na. 1**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa, watahiniwa 15,854 sawa na asilimia 2.99 walifaulu kwa kiwango kizuri cha alama 7 - 10; watahiniwa 327,013 (61.77%) walifaulu kwa kiwango cha wastani cha alama 3 - 6; na watahiniwa 186,570 (35.24%) walifaulu kwa kiwango hafifu cha alama 0 - 2.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika vipengele vingi vya swali hili unaonesha kuwa wanafunzi 327,013 sawa na asilimia 61.77 walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kutokuwa na umahiri wa kutosha wa dhana mbalimbali zilizotahiniwa kwa baadhi ya vipengele. Watahiniwa hao walimudu kuchagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele 3 hadi 6 na kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa 15,854 sawa na asilimia 2.99 walijibu vizuri swali hili kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha wa dhana mbalimbali zilizotahiniwa katika mada husika. Watahiniwa hao walichagua kwa usahihi herufi ya jibu sahihi katika vipengele vingi au vyote hivyo kuwa na ufaulu mzuri wa alama 6.5 hadi 10. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi vipengele (i) – (x) na kupata alama zote 10.


01. i/ C
ii/ D
iii/ E
iv/ B
v/ C
vi/ E
vii/ D
viii/ D
ix/ B
x/ E

**Kielelezo Na. 1.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 1

Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili kutokana na kuwa na umahiri wa mada mbalimbali zilizopimwa katika vipengele vyote.

Aidha, watahiniwa 186,570 sawa na asilimia 35.24 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama kati ya 0 na 2.5. Ufaulu huu ulitokana na kuchagua na kujibu kwa usahihi vipengele vichache (1-2) au kushindwa kujibu kipengele hata kimoja cha swali hili. Baadhi ya watahiniwa walichagua herufi za majibu yasiyo sahihi kutokana na kukosa maarifa ya kutosha ya dhana mbalimbali zilizotahiniwa. Uchambuzi zaidi wa namna watahiniwa hao walivyojibu vipengele mbalimbali vya swali hili umefafanuliwa kama ifuatavyo:

(i) *Katika masimulizi ya hadithi, maana sahihi ya soga ni ipi?*

*A Hadithi ndefu zinazohusu binadamu.*
*B Hadithi zinazohusu binadamu na wanyama.*
*C Hadithi fupi za kuchekesha na kukejeli.*
*D Hadithi fupi zinazoelezea makosa na uovu.*
*E Hadithi ndefu za kubuni na zinazochekesha.*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* hususani mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi.* Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kuelewa maana sahihi ya soga kama kipera cha utanzu wa hadithi katika fasihi simulizi. Watahiniwa waliojibu kwa usahihi swali hili walichagua herufi sahihi C *Hadithi fupi za kuchekesha na kukejeli* kwa kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu tanzu na vipera vya fasihi simulizi.

Watahiniwa wangine walichagua vipotoshi *A Hadithi ndefu zinazohusu binadamu*; *B Hadithi zinazohusu binadamu na wanyama*; *D Hadithi zinazoelezea makosa na uovu*; na *E Hadithi ndefu za kubuni na zinazochekesha*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa walishindwa kung'amua kuwa soga ni *hadithi fupi za kuchekesha na kukejeli*. Uchaguzi wa kipotoshi A ulitokana na kukosa uelewa kuwa hadithi ndefu zinazohusu binadamu ni *ngano*; uchaguzi wa kipotoshi B ulitokana na kutoelewa kuwa hadithi zinazohusu binadamu na wanyama ni *visasili***.** Aidha, uchaguzi wa kipotoshi D ulitokana na kukosa uelewa kuwa hadithi zinazoelezea makosa au uovu ni *vigano*; na uchaguzi wa kipotoshi E ulitokana na kukosa uelewa kuwa hadithi ndefu za kubuni na zinazochekesha ni *tarihi.* Uchaguzi wa vipotoshi hivi ulitokana na watahiniwa hao kuchanganya maana za dhana hizo kwa kuwa zote zinazoelezea vipera vya hadithi.

(ii) *Kati ya methali zifutazo ipi ina maana* ***tofauti*** *na zingine?*

*A Ujanja mwingi mbele giza.*
*B Akili nyingi huondoa maarifa.*
*C Mdharau biu huibuka yeye.*
*D Ukupigao ndio ukufunzao.*
*E Mdharau mwiba, mguu huota tende.*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* hususani mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi*. Swali lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa kuhusu methali na maana zake. Mtahiniwa alitakiwa kuchagua methali moja yenye maana tofauti na zingine kati ya methali tano alizopewa katika machaguo A hadi E. Watahiniwa waliojibu kwa usahihi swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi *D Ukupigao ndio ukufunzao* kwa kuwa methali hiyo humaanisha kuwa *mambo magumu yampatayo mtu*

*maishani huwa kama funzo kwake* au *anayekurudi au kukukemea ndiye anayekupenda*.

Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa walionesha kutokuwa na uelewa wa kutosha wa maana za methali hivyo kuchagua vipotoshi *A Ujanja mwingi mbele giza*; *B Akili nyingi huondoa maarifa*; *C Mdharau biu huibuka yeye*; na *E Mdharau mwiba, mguu huota tende.* Watahiniwa hawakuelewa kuwa methali katika vipotoshi hivyo zina maana sawa, zenye kutoa tahadhari kwa mtu anayejifanya mjuaji wa kila kitu, ambaye hatambui kuwa vipo asivyovijua na asipokuwa makini huweza kuingia kwenye matatizo au madhara makubwa.

(iii) *"Kiangazi kiliunguza kikaunguza ……. Hatimaye, mwaka elfu moja mia tisa hamsini na tisa mvua zikaanza japo kwa maringo*" usimulizi huu ni aina gani ya hadithi?

*A* *Visasili*
*B* *Vigano*
*C* *Soga*
*D* *Ngano*
*E* *Tarihi*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* hususani mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi*. Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu aina mbalimbali za masimulizi. Watahiniwa waliojibu kwa usahihi swali hili walichagua herufi *E Tarihi,* aina ya hadithi zinazoelezea matukio ya kihistoria yaliyowahi kutokea katika jamii fulani. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za hadithi.

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa walionesha kukosa uelewa wa aina za hadithi hivyo kuchagua vipotoshi *A Visasili*, *B Vigano, C Soga na D Ngano*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo haukuwa sahihi kwani *Visasili* huwa ni hadithi zinazotumia wahusika mbalimbali kuelezea asili ya vitu au watu; *Vigano* ni aina ya hadithi fupi zinazoeleza uovu wa watu kwa kusudi la kuwaadilisha; *C Soga* ni aina ya hadithi fupifupi zenye ucheshi zinazosimuliwa kwa nia ya kukejeli; na *D Ngano* ni aina ya hadithi zinazosimuliwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine ili kuwaasa watu hasa vijana kuhusu maisha na maadili ya jamii husika. Kwa ujumla, watahiniwa hawakuwa na maarifa kuhusu aina za hadithi.

(iv) "*Papai limeiva nyumbani lakini nashindwa kulila*" Kauli hii inawakilisha aina gani ya semi?

*A* *Methali.*
*B* *Mizungu.*
*C* *Nahau.*
*D* *Kitendawili.*
*E* *Misemo.*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* hususani mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Vipera vya Tanzu za Fasihi Simulizi*. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kutambua kauli za semi mbalimbali zinazotumika katika fasihi simulizi. Watahiniwa waliojibu kwa usahihi swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi *B Mizungu* kwani ndio dhana sahihi inayowakilishwa na kauli ya swali hili. Watahiniwa hao walionesha kuwa na umahiri wa kutosha kuhusu *mizungu* inayoelezwa kama *kauli zinazotumia lugha ya picha na mafumbo ili kuelezea vipengele mbalimbali vya mila na desturi za jamii fulani na mara nyingi hutumika katika miviga ili kufunza miiko ya jamii hiyo.*

Kwa upande mwingine, watahiniwa walioshindwa kujibu swali hili walichagua vipotoshi *A Methali*, *C Nahau*, *D Kitendawili* na *E Misemo* kutokana na kukosa uelewa wa kutosha kuhusu aina za semi. Watahiniwa hao hawakutambua kuwa *methali* ni semi fupi zenye mpangilio maalum wa maneno ambao hueleza kwa muhtasari na mafumbo mawazo mazito yanayotokana na uzoefu wa kijamii *nahau* ni kauli fupifupi zinzotumia lugha ya picha na ambazo hutumia maneno ya kawaida lakini hutoa maana tofauti na maana ya msingi ya maneno hayo; *kitendawili* ni kauli zinazotumia lugha ya picha/mafumbo na zenye kuhitaji majibu; na *misemo* ni vifungu vya maneno yanayotumiwa na jamii kwa namna maalumu ili kutoa maana inayoafiki ukweli fulani.

(v) *Mbinu ya kufipisha maneno katika ushairi ili kupata ulinganifu wa mizani huitwaje?*

*A* *Tafsida*
*B* *Tathlitha*
*C* *Inkisari*
*D* *Ufupisho*
*E* *Inkishafi*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Simulizi* hususani mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi*. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kutambua mbinu za kufupisha maneno katika ushairi ili kupata ulinganifu wa mizani. Watahiniwa waliojibu kwa usahihi swali hili walichagua herufi ya jibu *C Inkisari*.

Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili walichagua vipotoshi *A Tafsida*, *B Tathilitha*, *D Ufupisho*, na *E Inkishafi* kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu *uhakiki wa kazi za fasihi simulizi*. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa *inkisari* ndio mbinu ya kufupisha maneno katika ushairi ili kupata ulinganifu wa mizani. Watahiniwa hawakubaini kuwa t*afsida* ni mbinu ya kisanaa inayotumika kupunguza ukali wa maneno; *tathilitha* ni aina ya mashairi yaliyoundwa kwa mistari mitatu; *ufupisho* ni maelezo yaliyofupishwa kutokana na habari fulani ambayo kwa kawaida huwa ni ndefu; na *Inkishafi* ni jina la utenzi maarufu wa Kiswahili. Uchaguzi wa vipotoshi kwa ujumla ulitokana na watahiniwa hao kukosa uelewa wa mbinu za ulinganifu wa mizani katika ushairi.

(vi) *Ubainishaji wa maneno ya kuzua au yasiyo rasmi katika lugha huhusisha alama ipi ya uandishi kati ya hizi*?

A *Mkato*
B *Nukta-pacha*
C *Nukta*
D *Nukta-mkato*
E *Mtajo*

Swali lilitoka katika mada ya *Uandishi wa Insha* na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kubaini alama sahihi ya uandishi katika maneno ya kuzua au yasiyo rasmi katika lugha. Watahiniwa waliojibu kwa usahihi swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi *E Mtajo*. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha wa matumizi ya alama za uandishi.

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa walionesha kukosa umahiri kuhusu alama sahihi ya uandishi inayotumika kuonesha maneno ya kuzua au yasiyo rasmi katika lugha hivyo kuchagua vipotoshi *A Mkato, B Nukta*

*pacha*, *C Nukta,* na *D Nukta-mkato*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na watahiniwa hao kushindwa kuelewa kuwa alama ya *mkato* ni pumziko fupi katika sentensi; *nukta-pacha* ni alama inayoashiria maneno yaliyo katika orodha; *nukta* ni alama inayofanya kazi ya kukamilisha sentensi na kuonesha ufupisho wa maneno; na *nukta-mkato* ni alama inayofanya kazi ya kuunganisha sentensi kamili zaidi ya moja.

(vii) *Maneno yafuatayo yana maana zaidi ya moja* ***isipokuwa***

*A* *Ua.*
*B* *Mbuzi.*
*C* *Kata.*
*D* *Nyau.*
E *Paa.*

Swali hili lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali* hususani mada ndogo ya *Utata katika Mawasiliano. Swali* lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa kuelewa maneno yenye maana zaidi ya moja. Watahiniwa waliojibu kwa usahihi swali hili walikuwa na uelewa wa kutosha hivyo kuchagua herufi ya jibu sahihi *D Nyau*, ambalo ni neno lenye maana moja tu ya *mnyama paka* kati ya maneno waliyopewa.

Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa waliojibu swali hili walishindwa kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu maana mbalimbali za maneno hivyo kuchagua vipotoshi *A Ua*, *B Mbuzi*, *C Kata*, na *E Paa*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na watahiniwa kushindwa kuelewa kuwa maneno hayo yote yana maana zaidi ya moja ambapo *ua* ni kitendo cha kutoa uhai au sehemu ya mmea inayochanua; *mbuzi* ni kifaa cha kukunia nazi au mnyama jamii ya swala; *kata* ni kupitisha kitu chenye makali au chombo kinachotengenezwa kutokana na kifuu cha nazi au kibuyu na kutiwa mpini; na *paa* ni kitendo cha kuondoa magamba ya samaki kwa kuparuza kwa kitu, au kitendo cha kwenda angani.

(viii) *Katika neno 'umempelekea' mofimu ipi inawakilisha kauli ya kutendea?*

*A* *Me-*
*B* *–e-*
*C* *–m-*
*D* *–pelek-*
*E* *-a*

Swali lilitoka katika mada ya *Uundaji wa maneno* hususani mada ndogo *ya Kutumia Uambishaji* na lililenga kupima umahiri wa watahiniwa kubainisha mofimu inayowakilisha kauli ya kutendea. Watahiniwa waliojibu kwa usahihi swali hili walichagua herufi ya jibu sahihi *B -e-* hivyo kudhihirisha kuwa walikuwa na umahiri wa kutosha wa kubainisha kauli mbalimbali za vitenzi zilizodokezwa na mofimu walizopewa, hususani kauli ya kutendea.

Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa walikosa uelewa wa kauli mbalimbali za vitenzi zilizodokezwa na mofimu walizopewa hivyo kuchagua vipotoshi *A -me-*, *C m-, D -pelek-*, na *E -a*. Uchaguzi wa kipotoshi -*me*- ulitokana na watahiniwa hao kutoelewa kuwa *me*- ni mofimu ya hali timilifu katika kitenzi. Mofimu *m*- katika kitenzi huonesha mtenda wa jambo. Mofimu -*pelek*- ni mzizi wa neno *umempelekea*; na uchaguzi wa kipotoshi E -*a* ulitokana na watahiniwa kutoelewa kuwa -a ni irabu ishirizi na si mofimu ya kauli ya kutendea.


(ix) Kulingana na chimbuko la Kiswahili, lahaja ya Kijomvu ilizungumzwa maeneo gani?

*A* *Kaskazini mwa Tanga*
*B* *Kusini mwa Somalia*
*C* *Kisiwa cha Mafia*
*D* *Kisiwa cha Pemba*
E *Sehemu ya Malindi*

Swali lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* hususani mada ndogo ya *Asili ya Kiswahili*. Swali lililenga kupima umahiri wa watahiniwa kubainisha maeneo ambayo lahaja ya Kijomvu inazungumzwa. Watahiniwa waliojibu kwa usahihi swali hili walionesha kuwa na umahiri wa kutosha kuhusu lahaja za Kiswahili hivyo kuchagua herufi ya jibu sahihi *E Sehemu ya Malindi* ambako ndiko lahaja ya inazungumzwa.

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa walikosa maarifa kuhusu eneo ambako lahaja ya Kijomvu huzungumzwa, hivyo kuchagua vipotoshi *A Kaskazini mwa Tanga*, *B Kusini mwa Somalia*, *C Kisiwa cha Mafia,* na *D Kisiwa cha Pemba*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo ulitokana na watahiniwa hao kutoelewa kuwa *Kaskazini mwa Tanga* inazungumzwa lahaja ya Kimtang'ata, *Kusini mwa Somalia* inazungumzwa lahaja ya Chimiini,

*Kisiwa cha Mafia* kunazungumzwa lahaja ya Kimafia; na *Kisiwa cha Pemba* huzungumzwa lahaja ya Kipemba. Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili na kupata alama hafifu.



1 (i) D
(ii) C
(iii) C
(iv) E
(v) D
(vi) B
(vii)
(viii) A
(ix) D
(x) D

**Kielelezo Na. 1.2**: Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 1

Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi vipengele vyote vya swali hili kutokana na kukosa uelewa wa dhana anuwai za mada zilizotahiniwa katika swali la 1 (i) hadi (x) na kupata 0.


### 2.1.2 Swali la 2: Kuoanisha

Swali hili lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali* hususani mada ndogo ya *Utata katika Mawasilianao* na lililenga kupima maarifa ya watahiniwa kuhusu utata katika mawasiliano. Swali lilimtaka mtahiniwa kuoanisha tungo tata zilizopo katika Orodha A na chanzo cha utata huo kutoka Orodha B kisha kuandika herufi ya jibu sahihi katika kijitabu chake cha kujibia. Swali liliuliza:

> *Oanisha tungo tata zilizopo katika Orodha* A *na chanzo cha utata huo kutoka Orodha B, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kijitabu chako cha kujibia.*

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| *(i) Nilipofika nyumbani nilimkuta hayupo.*<br>*(ii) Juma alikimbizwa hospitalini.*<br>*(iii) Bwana Musa anaendesha.*<br>*(iv) Aliamua kumkimbilia siku ya mwaka mpya.*<br>*(v) Mama Halima amekuja.*<br>*(vi) Alikuwa na vitu vya dhamani nyingi.* | *A Tafsiri ya neno kwa neno*<br>*B Kutozingatia mantiki*<br>*C Kutumia mofimu ya kauli ya utendea*<br>*D Kutozingatia alama za uandishi*<br>*E Kutozingatia matamshi sahihi*<br>*F Kutumia mofimu ya kauli ya kutendeka*<br>*G Kutozingatia muktadha* |

Watahiniwa 529,437 sawa na asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani, ambapo watahiniwa 263,935 sawa na asilimia 49.85 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Aidha, watahiniwa 265,502 sawa na asilimia 50.15 walikuwa na ufaulu hafifu. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*

Chati Na. 2 inaonesha kuwa watahiniwa 81,805 sawa na asilimia 15.45 walifaulu kwa kiwango kizuri cha alama 4 – 6; watahiniwa 182,130 (34.40%) walifaulu kwa kiwango cha wastani cha alama 2 - 3; na

watahiniwa 265,502 (50.15%) walifaulu kwa kiwango hafifu cha alama 0 - 1.

Zaidi ya nusu ya watahiniwa 265,502 sawa na asilimia 50.15 waliojibu swali hili walipata alama za chini kati ya 0 na 1 kutokana na kukosa maarifa ya kutosha ya matumizi ya lugha hususani chanzo cha utata katika mazungumzo. Watahiniwa hao walishindwa kuoanisha kwa usahihi tungo tata zilizopo katika Orodha A na vyanzo vya utata huo kutoka Orodha B kutokana na kukosa umahiri wa matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alioanisha isivyo katika kipengele: (i) *Nilipofika nyumbani nilimkuta hayupo* kwa kuchagua kipotoshi *E Kutozingatia matamshi sahihi* badala ya B Kutozingatia mantiki; (ii) *Juma alikimbizwa hospitalini*, alichagua kipotoshi *B Kutozingatia mantiki* badala ya A Tafsiri ya neno kwa neno; (iii) *Bwana Musa anaendesha* alichagua kipotoshi *C Kutumia mofimu ya kauli ya utendea* badala ya *G* Kutozingatia muktadha; (iv) *Aliamua kumkimbilia siku ya mwaka mpya;* alichagua kipotoshi *D Kutozingatia alama za uandishi* badala C Kutumia mofimu ya kauli ya utendea; (v) *Mama Halima amekuja* alichagua kipotoshi *A Tafsiri ya neno kwa neno* badala ya D Kutozingatia alama za uandishi; na (vi) *Alikuwa na vitu vya dhamani nyingi;* alichagua kipotoshi *G Kutozingatia muktadha* badala ya E Kutozingatia matamshi sahihi. Kwa ujumla, watahiniwa wa kundi hili walichanganya vyanzo vya utata, hivyo kupata vipengele vichache au kushindwa kabisa kuoanisha kipengele hata kimoja na kupata 0. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali hili.

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | Orodha A | i | ii | iii | iv | v | vi |
| | Orodha B | E | C | F | A | B. | D |

**Kielelezo Na. 2.1:** Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 2

Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuoanisha tungo tata zilizopo katika *Orodha A* na vyanzo vya utata huo kutoka *Orodha B* kutokana na kutokuwa na umahiri kuhusu dhana mbalimbali zilizo na utata katika mawasiliano.

Aidha, watahiniwa 182,130 sawa na asilimia 34.40 waliofanya swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kati ya 2 na 3. Watahiniwa hao walioanisha kwa usahihi baadhi ya tungo tata zilizopo katika Orodha A na vyanzo vya utata huo kutoka Orodha B kwa kuandika herufi za majibu sahihi katika baadhi ya vipengele na kushindwa katika vipengele vingine, hivyo kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichagua herufi za majibu sahihi katika vipengele *(iv) C Kutumia mofimu ya utendea*, *(v) D Kutozingatia alama za uandishi,* na (vi) *E Kutozingatia matamshi sahihi*. Hata hivyo, mtahiniwa huyo alishindwa kutambua vyanzo vya utata katika vipengele (i), (ii) na (iii) kwa kuandika: *A Tafsiri ya neno kwa neno, F Kutumia mofimu ya utendeka* na *B Kutozingatia mantiki* badala ya herufi za majibu sahihi *(i) B Kutozingatia mantiki*, *(ii) A Tafsiri ya neno kwa neno*, na *(iii) G Kutozingatia muktadha*; hivyo kupata alama 3 kati ya alama 6 za swali hili.

Kwa upande mwingine, asilimia 15.45 sawa watahiniwa 81,805 walionesha kuwa na umahiri wa kutosha wa mada ya *Matumizi ya Lugha katika Muktadha Mbalimbali* hususani mada ndogo ya *Utata katika Mawasiliano*. Watahiniwa hao walioanisha tungo tata zilizopo katika Orodha A na vyanzo vya utata huo kutoka Orodha B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika vipengele 4 - 6. kwa usahihi, hivyo kupata alama za juu 4 - 6. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama za juu.

| | |
|---|---|
| 2 | (i) B |
| | (ii) A |
| | (iii) G |
| | (iv) C |
| | (v) D |
| | (vi) E |

**Kielelezo Na. 2.2**: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 2

Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama zote kwa kuoanisha vipengele vyote yaani (i) hadi (vi) kwa usahihi.

## 2.2 SEHEMU B: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

Sehemu hii ilikuwa na maswali sita (6) ya majibu mafupi na yenye jumla ya alama 54. Sehemu ilihusu mada za *Uundaji wa Maneno*, *Aina za Maneno*, *Maendeleo ya Kiswahili*, *Uandishi wa Insha za Hoja*, na *Ufahamu*.

### 2.2.1 Swali la 3: Tabia za Vitenzi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uundaji wa Maneno* hususani mada ndogo ya *Tabia za Vitenzi* na lililenga kupima maarifa aliyonayo mtahiniwa kuhusu hali timilifu za vitenzi vya Kiswahili. Swali lilikuwa na vipengele (a) na (b), ambapo kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kuandika sentensi alizopewa katika hali timilifu; na kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kubainisha njeo sahihi katika tungo alizopewa.


Watahiniwa 529,437 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali lilikuwa na ufaulu wa wastani ambapo watahiniwa 306,160 sawa na asilimia 58.39 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri na watahiniwa 220,227 sawa na asilimia 41.61 walikuwa na ufaulu hafifu. Jedwali Na. 2 linaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kiasilimia.

**Jedwali Na. 2: Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa**

| Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0.0 - 2.5 | 220,227 | 41.61 |
| 3.0 - 5.5 | 196,543 | 37.12 |
| 6.0 - 9.0 | 112,617 | 21.27 |

Jedwali Na. 2 linaonesha kuwa, watahiniwa 112,617 sawa na asilimia 21.27 walifaulu kwa kiwango kizuri cha alama 6 – 9; watahiniwa 196,543 (37.12%) walifaulu kwa kiwango cha wastani cha alama 3 – 5.5; na watahiniwa 220,227 (41.61%) walifaulu kwa kiwango hafifu cha alama 0 – 2.5.

Watahiniwa 220,227 (41.61%) waliofanya mtihani huu walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama kati ya 0 na 2.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kukosa maarifa ya kutosha ya uambishaji, hivyo kutoandika sentensi walizopewa katika hali timilifu katika kipengele (a) (i) hadi (v) na kushindwa kubainisha njeo sahihi katika tungo walizopewa katika kipengele (b) (i) hadi (viii). Baadhi ya watahiniwa walidondosha baadhi ya maneno katika sentensi badala ya kuandika sentensi hizo katika hali timilifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kuandika kwa usahihi vipengele vyote viwili na badala yake, aliandika ukanushi katika sentensi alizopewa kwa kuandika katika kipengele (a) (ii) *Mimi sitamshinda Rashidi kwa mbio* na (iii) *Wewe si abiria lakini lazima ulipe nauli* badala ya kuandika sentensi hizo katika hali timilifu. Pia, katika kipengele (b) alishindwa kubainisha njeo sahihi kwa kuandika (i) *Asha hafagii jikoni*, (ii) *Mwalimu hafundishi kuimba*, (iii) *John hakuwa amefika stendi* (iv) *Watoto wake hawatamlilia sana*; majibu ambayo ni kinyume kabisa na matakwa ya swali hili. Mtahiniwa mwingine alishindwa kujibu swali hili katika kipengele (b) ambapo aliandika maelezo yasiyohusiana na njeo husika kama vile: (i) *Wakati wa mchana*, (ii) *Wakati wa kutoka shule*, (iii) *Wakati wa asubuhi*, (iv) *Wakati atakapokuwa hayupo*, na (v) *Wakati utakao kuja*, (vi) *Wakati wa uwanjani*, (vii) *Wakati wa usiku na mchana au kwa muda wote*, na (viii) *Wakati walipokuwa wanaongea*. Kwa ujumla, watahiniwa hao walikosa umahiri wa kuandika hali timilifu katika sentensi walizopewa kama vile (i) *Petro ha**ja**watembelea wazee wake likizo hii*; (ii) *Mimi ni**me**mshinda Rashidi kwa mbio*; (iii) Wewe u**me**kuwa abiria lakini lazima ulipe nauli, (iv) *Mchezaji a**me**rusha mpira*; na (v) *Mwalimu a**me**fundisha somo la Kiswahili*. Kipengele (b) walitakiwa kubainisha njeo sahihi katika tungo walizopewa kama ifuatavyo: (i) *wakati uliopo*; (ii) *wakati ujao*; (iii) *wakati uliopita timilifu*; (iv) *wakati ujao*; (v) *wakati ujao timilifu*; (vi) *wakati uliopita*; (vii) *wakati uliopo*; na (viii) *wakati uliopita timilifu*. Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili na kupata alama 0.




3a) Andika sentensi zifuatazo katika hali timilifu
i) Petro hatawatembelea wazee wake likizo hii
Petro kuwatembelea wazee wake kila likizo
ii) mimi ninamshinda Rashidi kwa mbio
Sisi tunamshinda rashidi kwa mbio
iii) wewe ni abiria lakini lazima ulipe nauli
wao ni abiria lakini lazima walipe nauli
iv) mchezaji anarusha mpira
nafsi ya kwanza umoja
yeye anarusha mpira
v) mwalimu anafundisha somo la kiswahili
mwalimu Mufundisha somo la kiswahili
3)B Bainisha njeo sahihi katika tungo
i) Asha anafagia sikoni
N T E
ii) mwalimu atafundisha kuimba
N T V
iii) John alikuwa wamefika stendi
N T TS N
iv) watoto wake watamlilia sana
N V T E
v) hapo nitakuwa nimeondoka
V t T
vi) Timu yetu ilicheza vizuri sana
N V T E
vii) Askari wanalinda raia
N N N
viii) watoto walikuwa wanaturahisha
N T E

**Kielelezo Na. 3.1**: Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 3

Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyebadili nafsi kutoka hali ya umoja kwenda wingi katika kipengele (a) na kubainisha aina za maneno katika kipengele (b) badala ya kuandika hali timilifu za sentensi na kubainisha njeo katika tungo mtawalia.

Aidha, watahiniwa 196,543 sawa na asilimia 37.12 waliojibu swali hili walipata alama za wastani kati ya 3 na 6. Ufaulu huu wa kiwango cha wastani ulitokana na watahiniwa hao kutoa majibu yasiyojitosheleza katika vipengele (a) na (b). Wapo watahiniwa waliojibu kipengele kimoja na kushindwa kingine. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alishindwa kuandika sentensi alizopewa katika hali timilifu katika kipengele (a) lakini alibainisha kwa usahihi njeo katika tungo walizopewa na kupata alama za wastani.

Hata hivyo, wapo watahiniwa waliojibu vizuri swali hili ambapo, watahiniwa 112,617 sawa na asilimia 21.27 walikuwa na ufaulu mzuri kwa kupata alama kati ya 6 na 9. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuwa na umahiri wa kutosha wa dhana ya uambishaji, hivyo kuandika kwa usahihi sentensi walizopewa katika hali timilifu. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama za juu.





**Kielelezo Na. 3.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 3

Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali kwa kujibu kwa usahihi vipengele vyote vya swali hili (a) na (b).

### 2.2.2 Swali la 4: Uambishaji

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uundaji wa Maneno* hususani mada ndogo ya *Kutumia Uambishaji* na lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu dhima za uambishaji katika lugha ya Kiswahili. Swali lilikuwa na vipengele (a) na (b), ambapo kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa aeleze dhima tano za uambishaji katika lugha ya Kiswahili. Kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kubainisha mzizi katika maneno aliyopewa.

Watahiniwa 529,437 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu, ambapo watahiniwa 337,759 sawa na asilimia 63.80 waliufaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Aidha, watahiniwa 191,678 sawa na asilimia 36.20 walifaulu kwa kiwango hafifu. Chati Na. 3 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kiasilimia.





**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4*

Chati Na. 3 inaonesha kuwa, watahiniwa 138,258 sawa na asilimia 26.12 walifaulu kwa kiwango kizuri cha alama 6 – 9; watahiniwa 199,501 (37.68%) walifaulu kwa kiwango cha wastani cha alama 3 – 5.5; na

watahiniwa 191,678 (36.20%) walifaulu kwa kiwango hafifu cha alama 0 – 2.5.

Asilimia 26.12 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa juu kwa kupata alama kati ya 6 na 9. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuonesha umahiri mkubwa kuhusu dhima za uambishaji katika tungo za lugha ya Kiswahili katika kipengele (a) na kubainisha kwa usahihi mzizi wa maneno waliyopewa katika kipengele (b). Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kipengele (a) alieleza kwa usahihi dhima tano za uambishaji katika lugha ya Kiswahili kama vile: (i) *kudokeza njeo*; (ii) *kudokeza nafsi*; (iii) *kudokeza kauli mbalimbali za vitenzi*; (iv) *kuonesha ukanushi*; na (v) *kuonesha urejeshi*. Katika kipengele (b) alibainisha kwa usahihi mizizi ya maneno aliyopewa kama ifuatavyo: (i) mwokozi - *oko*; (ii) matendo - *tend*; (iii) mlaji - *l*; na (iv) uonevu - *one*. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama za juu.



04. a) Dhima tano za uambishaji katika lugha ni;
i) Hutumika kudokeza njeo
Mfano - Alilia - wakati uliopita.
ii) Hutumika kudokeza nafsi.
Mfano : Walilima - Nafsi ya tatu wingi.
iii) Hutumika kudokeza kauli mbalimbali za vitenzi. Mfano kutenda, kutendwa.
iv) Huonesha ukanushi.
Mfano : Hachezi.
v) Huonesha urejeshi
Mfano aliyepigwa.
b) Kubainisha mzizi katika maneno yafuatayo.
i) Mwokozi
-oko-
ii) Matendo
-tend-
iii) Mlaji
-l-
iv) Uonevu
-one-

**Kielelezo Na. 4.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 4

Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kwa usahihi dhima tano za uambishaji na kubainisha kwa usahihi mzizi katika maneno aliyopewa hivyo kukidhi matakwa ya swali katika vipengele vyote viwili na kupata alama za juu.

Hata hivyo, asilimia 37.68 ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kwa kupata alama kati ya 3 na 5.5. Ufaulu wa wastani ulitokana na watahiniwa hao kukidhi sehemu ya matakwa ya swali kwa baadhi ya vipengele na kushindwa katika vipengele vingine. Katika kipengele (a), baadhi ya watahiniwa walishindwa kueleza kwa usahihi dhima tano za viambishi katika lugha ya Kiswahili na badala yake walieleza mambo tofauti tofauti yanayohusu lugha kama vile (i) *kukuza lugha ya Kiswahili*, (ii) *kuongeza misamiati ya lugha ya Kiswahili*, (iii) *husaidia katika kurahisisha na kuwezesha mawasiliano*, (iv) *kupamba lugha ya Kiswahili*, na (v) *kuunda maneno mapya katika lugha*. Hata hivyo, katika kipengele (b), watahiniwa wengi walibainisha kwa usahihi mizizi ya maneno yote waliyopewa hivyo kupata alama za wastani.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 36.20 ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama kati ya 0 na 2.5. Miongoni mwao, asilimia 9.30 walipata alama 0 kutokana na kushindwa kueleza dhima tano za uambishaji katika lugha Kiswahili katika kipengele (a). Pia, katika kipengele (b), walishindwa kubainisha mizizi ya maneno waliyopewa na kupata alama 0. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika katika kipengele (a) faida za kamusi kama vile: (i) *Husaidia kuelewa neno* na (iii) *Husaidia kujua mzizi wa neno uko wapi*; majibu ambayo hayakidhi matakwa ya swali badala ya kueleza dhima anuwai za uambishaji kama vile (i) *kudokeza njeo*; (ii) *kudokeza nafsi*; (iii) *kudokeza kauli mbalimbali za vitenzi*; (iv) *kuonesha ukanushi*; na (v) *kuonesha urejeshi*. Katika kipengele (b) alishindwa kubainisha kwa usahihi mizizi ya maneno aliyopewa kwa kuandika: (i) **mwokozi –o-** badala ya -*oko*-, (ii) **matendo –e-** badala ya -tend-, (iii) **mlaji** –**la-** badala ya -l-, na (iv) **uonevu** –**ne-** badala ya -one-. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili.




**Kielelezo Na. 4.2:** Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 4


Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza dhima za fasihi/lugha badala ya dhima za uambishaji katika lugha ya Kiswahili. Pia, katika kipengele (b), alibainisha mzizi wa neno isivyo sahihi na kupata 0.

### 2.2.3 Swali la 5: Utata katika Mawasiliano

Swali hili lilitoka katika mada ya *Utumizi wa Lugha* hususani mada ndogo ya *Utata katika Mawasiliano* na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kubaini visawe vya maneno pamoja na kueleza maana za msingi na za ziada za maneno aliyopewa. Swali lilikuwa na vipengele (a) na (b) ambapo, kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kuandika visawe vya maneno aliyopewa kisha kutunga sentensi moja kwa kila kisawe; na kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kueleza maana ya msingi na ya ziada ya maneno aliyopewa.

Watahiniwa 529,437 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango cha chini zaidi cha ufaulu, ambapo watahiniwa 384,609 sawa na asilimia 72.64 walifaulu kwa kiwango hafifu. Aidha, watahiniwa 144,828 sawa na asilimia

27.36 pekee ndio walikuwa na ufaulu wa wastani hadi mzuri. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kiasilimia.





**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5*

Chati Na. 4 inaonesha kuwa, watahiniwa 12,799 sawa na asilimia 2.42 walifaulu kwa kiwango kizuri cha alama 6 – 9; watahiniwa 132,029 (24.94%) walifaulu kwa kiwango cha wastani cha alama 3 – 5.5; na watahiniwa 384,609 (72.64%) walifaulu kwa kiwango hafifu cha alama 0 – 2.5.

Robo tatu ya watahiniwa (384,609) sawa na asilimia 72.64 ya wote waliojibu swali hili walikosa umahiri wa kubainisha na kutunga sentensi visawe vya maneno waliyopewa katika kipengele (a) (i) hadi (v). Pia, walishindwa kueleza maana za msingi na za ziada katika kipengele (b) (i) hadi (iv), hivyo kuwa na ufaulu hafifu. Watahiniwa hao walionesha kukosa uelewa kuhusu matumizi ya kamusi, hivyo baadhi walitunga sentensi kwa kutumia maneno hayo, na wengine waliandika vinyume vya maneno hayo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kujibu kipengele (a) aliandika (i) majaaliwa – *majanga*, (ii) sahihi – *isiyo sahihi*, (iii) sifuri – *namba*, (iv) chuchumaa – *simama*, na (v) choo – *sebule*, badala ya kuonesha visawe sahihi vya maneno hayo kama vile (i) kudura/mustakabali, (ii) sawa/sawasawa/barabara, (iii) ziro/bila/nunge, (iv) chutama/otama/totama na (v) msala/maliwato/haja mtawalia.

Aidha, katika kipengele (b), watahiniwa wengine walishindwa kueleza maana sahihi za msingi na za ziada katika maneno (i – iv) kwa kuandika mambo mbalimbali kama vile methali, nahau, misemo, na vitendawili vyenye kutumia maneno hayo kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika katika kipengele (b) (i) *mchumia juani hulia kivulini* na (ii) *hasidi hana sababu*, majibu yasiyokidhi matakwa ya swali hili. Watahiniwa hao walitakiwa kuandika katika kipengele (b) (i) **mchumi** - *mtu aliyesoma na anayejihusisha na uchumi* (maana ya msingi) na *mtu anayebania pesa/asiyetumia pesa ovyo* (maana ya ziada); (ii) **husudu** - *hali ya mtu kuwa na wivu* (msingi) na *kitendo cha kumfanyia mwenzake mabaya* (ziada); (iii) **kichaa** - *mtu asiye na akili timamu* (msingi) na *mtu asiyetulia sehemu moja* (ziada); na (iv) **mchafu** - *mtu asiyezingatia usafi wa mwili na nguo* (msingi) na *mtu asiye na maadili/hutukana ovyo* (ziada). Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali la 5 (b) na kupata alama hafifu.


5 (b) (i) Mchumi
Mzizi – chumi –
(ii) Husudu
Mzizi – usu –
(iii) Kichaa
Mzizi – k - ch
(iv) Mchafu
Mzizi – chafu –

**Kielelezo Na 5.1:** Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 5 (b)


Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyebainisha mzizi katika maneno (i – iv) kinyume na matakwa ya swali badala ya kueleza maana za msingi na za ziada katika maneno aliyopewa kama ilivyotakiwa.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 132,029 sawa na asilimia 24.94 ya waliofanya mtihani huu walikuwa na ufaulu wa wastani kwa kupata alama kati ya 3 na 6. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuandika kwa usahihi baadhi ya visawe vya maneno na kushindwa kufanya hivyo kwa maneno mengine. Watahiniwa hao waliandika kwa usahihi visawe vya maneno mawili au matatu na kushindwa katika maneno mengine. Vilevile,

walitunga sentensi sahihi kwa baadhi ya visawe na kushindwa kufanya hivyo kwa sentensi zingine. Pia, katika kipengele (b) waliandika kwa usahihi maana za msingi na za ziada kwa baadhi ya maneno na kushindwa katika maneno mengine, hivyo kupata alama za wastani.

Uchambuzi wa kina uliofanyika katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa 12,799 sawa na asilimia 2.42 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa juu na kupata alama kati ya 6 na 9. Ufaulu huo ulitokana na watahiniwa hao kuwa na umahiri wa kutosha wa matumizi ya kamusi. Watahiniwa waliandika kwa usahihi visawe vya maneno (i) *majaliwa*, (ii) *sahihi*, (iii) *sifuri*, (iv) *chuchumaa*, na (v) *choo* katika kipengele (a) kama ifuatavyo: (i) *majaliwa* - kudura/mustakabali, (ii) *sahihi* – sawa, sawasawa, barabara; (iii) *sifuri* – ziro, bila, nunge, (iv) *chuchumaa* – chutama, otama, totama na (v) choo - msala, maliwato au haja. Hata hivyo, watahiniwa hao walitunga sentensi sahihi kwa kila kisawe kama mtahiniwa mmoja alivyoandika: (a) (i) *Kudra – Tutafaulu kwa kudra za mwenyezi Mungu*; (ii) *Kweli – Umenena kweli juu ya jambo hili*; (iii) *Ziro – Hakuna mwanafunzi atakayepata alama ziro katika mtihani huu*; (iv) *Chutama – Watoto walichutama chini ya mti wenye kivuli*; na (v) *Uani – Wanadamu hujisaidia uani*.

Katika kipengele (b), watahiniwa hao walieleza kwa usahihi maana za msingi na za ziada za maneno: (i) *mchumi*, (ii) *husudu*, (iii) *kichaa*, na (iv) *mchafu* kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kwa usahihi maana za msingi na za ziada za maneno aliyopewa kama ifuatavyo: (i) **mchumi** maana ya msingi *ni mtu aliyesoma na anayejihusisha na uchumi*, na maana ya ziada *ni mtu anayebania pesa/asiyetumia pesa ovyo*. (ii) **husudu** maana ya msingi *ni hali ya mtu kuwa na wivu*, na maana ya ziada ni *kitendo cha kumfanyia mwenzake mabaya*; (iii) **kichaa** maana ya msingi ni *mtu asiye na akili timamu*, na maana ya ziada ni *mtu asiyetulia sehemu moja*; na (iv) **mchafu** maana ya msingi ni *mtu asiyezingatia usafi wa mwili na nguo*, na maana ya ziada ni *mtu asiye na maadili*. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.


5 (a) (i) Baraka
Hizi ni baraka kutoka kwa Mungu.
(ii) Barabara
Tunatakiwa kujibu maswali barabara kabisa.
(iii) Nunge
Amepata nunge katika jaribio hili.
(iv) Chutama
Kidonda kinanizuia kuchutama kiurahisi.
(v) Maliwato
Alikwenda maliwato kujisaidia.

(b) (i) Mtu anayejhusika na mambo ya kiuchumi na fedha
Mtu ~~anaye~~ mbahili.
(ii) Fanyia mtu jambo baya/husuda.
Kutanika na watu kwa jambo fulani.
(iii) Mtu aliyepungukiwa na akili
Mtu anayefanya mambo bila mpangilio.
(iv) Mtu asiye msafi kimuonekano.
Mtu mwenye tabia mbaya.


**Kielelezo Na. 5.2:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 5

Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vipengele vyote (a) na (b) kwa kukidhi matakwa ya swali na kupata alama za juu.

### 2.2.4 Swali la 6: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* hususani mada ndogo ya *Asili ya Kiswahili*. Swali lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa katika kuonesha namna lugha ya Kiswahili inavyofanana na lugha za Kibantu. Swali lilimtaka mtahiniwa kutumia hoja sita kuelezea kwa mifano namna lugha ya Kiswahili na lugha za Kibantu zinavyoshabihiana.

Watahiniwa 529,437 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali lilikuwa na ufaulu wa wastani, ambapo watahiniwa 281,063 sawa na asilimia 53.09 walifaulu kwa kiwango cha wastani hadi kizuri. Aidha, watahiniwa 248,374 sawa na asilimia 46.91 walikuwa na ufaulu hafifu. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Chati Na. 5 inaonesha kuwa, watahiniwa 125,144 sawa na asilimia 23.64 walifaulu kwa kiwango kizuri cha alama 6 – 9; watahiniwa 155,919 (29.45%) walifaulu kwa kiwango cha wastani cha alama 3 – 5.5; na watahiniwa 248,374 (46.91%) walifaulu kwa kiwango hafifu cha alama 0 – 2.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 248,374 sawa na asilimia 46.91 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 2.5. Watahiniwa hao walionesha kukosa umahiri katika mada ndogo ya chimbuko na asili ya Kiswahili, hivyo kushindwa kueleza kwa usahihi namna lugha ya Kiswahili na lugha za Kibantu zinavyoshabihiana. Miongoni mwao, asilimia 31.79 walipata 0 kwani hawakuwa na uelewa kabisa kuhusu mfanano uliopo kati ya lugha hizo. Baadhi ya watahiniwa waliorodhesha lugha kadhaa za Kibantu na wengine walitoa hoja mbalimbali zisizohusiana na kushabihiana kati ya lugha ya Kiswahili na lugha za Kibantu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja ambazo ni sababu za kukua/kuenea kwa lugha kama vile: (i) *mwingiliano wa kijamii*, (ii) *kuchangamana sehemu za mikusanyiko*, (iii) *kuhama makazi*, na (vi) *muingiliano katika ndoa*. Kwa ujumla, majibu ya watahiniwa hao hayakukidhi matakwa ya swali kwani walitakiwa kueleza kwa mifano namna lugha za Kibantu na Kiswahili zinavyofanana katika (i) *mpangilio wa maneno katika sentensi*, (ii) *upatanisho wa kisarufi kati ya kiima na kiarifu*, (iii) *mnyumbuliko wa vitenzi*, (iv) *miundo wa sentensi*, (v)

*msamiati wa msingi u,* na (vi) *miisho ya vitenzi vya Kiswahili na Kibantu*. Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili na kupata alama 0.

06. i. Uhabidi wa Marko Polo. Huyu ni mtu aliye gundua ukubwa na uzuri wa kisiwa cha zanzibar na katika maelezo yake alisema kuwamba " Zanzibar ni kisiwa chenye ukubwa wa maili mia mbili, watu wake wanampa mfalme wao, wanatumia lugha yao na hawalipi kodi"

ii. Uhabidi wa Al-Idrisi. Huyu ni mgunduzi aliyegundua jina la kwanza la zanzibar kuwa ni Zanjiba (unguja) pia aligundua majina ya ndizi yaliyotumika zamani kama ndizi sukari, mkono wa tembo, ndizi kikombe.

iii. Uhabidi wa Ibin-batuta. Huyu ni mtu aliye igawa pwani ya Afrika mashariki katika makundi matatu ambayo ni waarabu, waswahili na waafrika walipoungana wakaamua kutumia lugha moja ambayo ni kiswahili hii inathibitisha kuwa kiswahili ni kiswahili.

iv. Utenzi wa Fumo liyongo. Huu ni utenzi ambao uliandikwa na mfalme wa zamani japoku

iv. japokuwa lugha yake ni sanifu na lugha inayotumika sasa.

v. Historia ya kilwa. Mji wa kilwa ni mji ambao uliongozwa na masultani ambao watu wake wali wapa masultani hao majina ya utani kutokana na tabia zao sultani wa kwanza alipewa jina la "Mkoma watu" kutokana na tabia yake ya kupenda kupiga watu vichwani wakati wa mikutano ya baba yake.

**Kielelezo Na 6.1:** Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 6

Kielelezo Na 6.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeeleza ushahidi wa kihistoria kinyume na matakwa ya swali, ambao kiuhalisia hauwezi kuthibitisha ubantu wa Kiswahili bali hudhihirisha kuwepo kwa Kiswahili kabla ya kuja kwa wageni katika pwani ya Afrika Mashariki, hivyo kupata alama hafifu.

Hata hivyo, watahiniwa 155,919 sawa na asilimia 29.45 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kwa kupata alama kati ya 3 na 5.5. Ufaulu huu ulitokana na kutoa hoja zisizojitosheleza katika kuelezea namna lugha za Kibantu na Kiswahili zinavyoshabihiana. Pia, baadhi yao walitoa hoja pungufu na wengine walishindwa kutoa mifano sahihi katika hoja zao ili kuthibitisha mfanano uliopo kati ya lugha za Kibantu na Kiswahili, hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 125,144 sawa na asilimia 23.64 ya waliojibu swali hili walifanya vizuri na kupata alama za juu kati ya 6 na 9. Ufaulu huo ulitokana na watahiniwa hao kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kushabihiana kwa lugha za Kibantu na Kiswahili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alithibitisha kwa hoja zifuatazo: (i) *Mpangilio wa maneno katika sentensi za Kiswahili*, (ii) *Upatanisho wa kisarufi kati ya kiima na kiarifu*, (iii) *Mnyumbuliko wa vitenzi*, (iv) *Muundo wa sentensi za Kiswahili na kibantu huwa na muundo wa kiima na kiarifu*, (v) *Msamiati wa msingi hufanana katika Kiswahili na kibantu*, na (vi) *Miisho ya vitenzi vya Kiswahili na kibantu hufanana*. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

6 kueleza kwa mifano namna ambazo lugha ya kibantu na kiswahili vinavyoshahabiana.

(i) Msamiati wa Lugha.

ukifuatilia kwa makini msamiati wa lugha ya kiswahili unafanana sana na ule wa lugha za kibantu kwa kuwa una mzizi wa neno kama ule wa kiswahili Mfano.

Mfano.

| Lugha | Msamiati |
|---|---|
| kiswahili | kucheka |
| kimatengo | kuheka |
| kigogo | kuseka |
| kichagga | kuseksya |

(ii) Tungo za kiswahili

Tungo ni kipashio cha lugha chenye muundo wa kiima na kiarifu. kwa kuzichunguza tungo nyingi za lugha za kibantu zina muundo wa kiima yaani mtenda wa jambo na kiarifu yaani jambo linalotendeka. ambapo katika kiswahili, tungo lazima iwe na muundo wa kiima na kiarifu.

Mfano.


| Lugha | Tungo (sentensi) |
|---|---|
| kiswahili | Mama anakunywa maji |
| kimatengo | Amabu atendakunywa maso. |
| kichaggaa | Mai ainyo Mringa. |

(iii) Mnyambuliko katika vitenzi.

Vilevile katika unyambulishaji wa vitenzi kwa kupachika viambishi katika mizizi ya maneno, kauli za kutenda, kutendesha, kutendeka na kutendeana zimekuwa zikijitokeza katika lugha za kibantu kama zilivyozoeleka katika lugha ya kiswahili

Mfano

| | KAULI | | |
|---|---|---|---|
| Lugha | kutenda | kutendesha | kutendea. |
| kiswahili | kucheka | kuchekesha | kuchekelea, |
| kigogo | kuseka | kusekesa | kusekelela |
| kimatengo | kuheka | kuhekesa | kuhekelela |



(iv) Upatanisho wa kisarufi katika tungo.
Ni uhusiano uliopo katika kiima kinachotawala kitenzi katika kiarifu. katika tungo za kibantu na za kiswahili zote zinazingatia upatanisho wa kisarufi, ambapo mtenda katika kiima anashabihiana na kitenzi kilichopo katika kiarifu.

Mfano.

| Lugha | sentensi |
|---|---|
| kiswahili | Mama anakunywa maji (upatanisho wa kisarufi) |
| kimatengo | Amabu a-kunywa masa (upatanisho wa kisarufi) |
| kichagga | Mai a- inyo Mringa (upatanisho wa kisarufi) |

(v) Viambishi tata tamati maana katika vitenzi.
Hivi ni viambishi "a" vinavyopachikwa mwishoni mwa vitenzi ili kuleta maana. katika lugha ya kiswahili vitenzi vyote vinaishia na viambishi tamati maana "a", hivyo basi hata lugha za kibantu zina viambishi tamati maana "a" katika vitenzi vya kibantu.

Mfano

| Lugha | vitenzi |
|---|---|
| kiswahili | Anakul-a |
| kimatengo | Atendakul-a |
| kigogo | Akuly-a |
| kichagga | Akely-a |

(vi) Muundo wa kiarifu
katika lugha ya kiswahili kiarifu kinaweza kuundwa na kitenzi kikuu na kisaidizi, na nomino kama kikundi kitenzi, na kikundi nomino au kielezi. Ukichunguza kwa makini, muundo wa kiarifu wa lugha za kibantu umeundwa na kikundi kitenzi

mfano

| lugha | kiarifu. |
|---|---|
| kiswahili | Anakunywa (KT) maji (KN) |
| kimatengo | Akunywa (KT) masa (KN) |


**Kielelezo Na 6.2:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 6

Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetumia hoja sita kuelezea kwa usahihi namna lugha za Kiswahili na Kibantu zinavyoshabihiana na kutoa mifano sahihi, hivyo kukidhi matakwa ya swali na kupata alama zote tisa (9).

### 2.2.5 Swali la 7: Uandishi wa Insha

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uandishi*, hususani mada ndogo ya *Uandishi wa Insha za Hoja* na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kuunda dhana/mawazo mbalimbali yenye mantiki. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika insha yenye maneno yasiyopungua mia mbili (200) na yasiyozidi mia mbili na hamsini (250) kuhusu "*Umuhimu wa lishe bora kwa watoto*."

Watahiniwa 529,437 sawa na asilimia 100 ya wote waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili lilikuwa na ufaulu wa juu, ambapo watahiniwa 459,983 sawa na asilimia 86.88 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Aidha, watahiniwa wachache (69,454) sawa na asilimia 13.2 pekee ndio walikuwa na ufaulu hafifu. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*

Chati Na. 6 inaonesha kuwa, watahiniwa 295,297 sawa na asilimia 55.77 walifaulu kwa kiwango kizuri cha alama 6 – 9; watahiniwa 164,686 (31.11%) walifaulu kwa kiwango cha wastani cha alama 3 – 5.5; na watahiniwa 69,454 (13.12%) walifaulu kwa kiwango hafifu cha alama 0 – 2.5.


Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa watahiniwa 295,297 sawa na asilimia 55.77 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa juu kwa kupata

alama kati ya 6 na 9. Hii ni kutokana na watahiniwa hao kuonesha kuwa na umahiri wa kutosha wa kuandika insha kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa insha ya hoja. Watahiniwa hao waliandika kwa usahihi insha iliyokuwa na maneno mia mbili (200) hadi mia mbili na hamsini (250) kuhusu ''*Umuhimu wa lishe bora kwa watoto*". Watahiniwa walizingatia taratibu za uandishi wa insha kama vile: kichwa cha insha (kilichoandikwa kwa herufi kubwa), utangulizi, kiini cha insha, mwisho wa insha, na kuzingatia alama za uandishi, matumizi ya lugha sanifu, na idadi stahiki ya maneno. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika insha iliyokidhi matakwa ya swali kwa kuandika *kichwa cha habari kwa herufi kubwa, utangulizi mzuri aliotoa muhtasari wa lishe bora* na katika kiini alitoa hoja nzuri zinazoelezea umuhimu wa lishe bora kwa watoto kama vile: *kuongeza nguvu mwilini*, *kulinda kinga ya mwili*, *kukua kimwili na kiakili*, *kujikinga na magonjwa*, na *kuongeza afya ya mwili*. Pia, mtahiniwa huyo aliandika hitimisho zuri linaloendana na insha yake. Kwa ujumla, mtahiniwa huyo aliandika insha iliyozingatia alama za uandishi, matumizi ya lugha sanifu na idadi sahihi ya maneno (239) kulingana na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika insha kwa usahihi ma kupata alama za juu.

7. UMUHIMU WA LISHE KWA WATOTO

Lishe bora ni lishe yenye mchanganyiko wa makundi mbalimbali ya vyakula katika viwango vinavyotakiwa. makundi hayo ni protini, vitamini, kabohaidreti maji na madini. Lishe bora ni muhimu kwa watoto hasa walio na umri wa kuanzia miaka mitano kama inavyoelezwa hapa chini.

Ukuaji wa miili ya watoto; Lishe bora husaidia katika ukuaji wa kasi wa miili ya watoto kwa maana kwamba huongeza kasi ya kuzaliana kwa seli mwilini. Kundi la vyakula vinavyohusika na ukuaji wa mwili ni protini. mfano watoto wa ulaya hukua haraka kwa sababu ya lishe bora.


Kujikinga na magonjwa; Lishe bora hupa mwili uwezo wa kujikinga na magonjwa kwani huimarisha kinga ya mwili. vyakula vya vitamini kama vile matunda, mbogamboga na maziwa husaidia kuimarisha kinga ya mwili. Mfano watoto wa ulaya hawaumwi hovyohovyo kwa sababu ya lishe bora.

Huipa mwili nguvu, nishati na joto; watoto wakipatiwa vyakula vya kabohaidreti kama ugali, wali, nazi, mahindi, ngano na sukari hupata mili yenye nguvu na joto na hivyo huweza kushiriki katika kazi za mikono kikamilifu na kupelekea maendeleo

Hupanua uwezo wa kufikiri na ubunifu; watoto wakipatiwa lishe bora, fahamu na akili zao huimarishwa na kupanuliwa. vilevile uwezo wao wa kufikiri kabla ya kufanya maamuzi huwa ni mkubwa. mfano kula vyakula vya protini

Huongeza nguvu kazi ya taifa; Hii ni kwa sababu lishe bora hupunguza kasi ya vifo vitokanavyo na magonjwa yaliyosababishwa na lishe duni kama utapiamlo, kwashakoo. Hii husaidia katika maendeleo ya nchi.

Hata hivyo, licha ya juhudi za serikali na vyombo binafsi katika kuhakikisha lishe bora inatolewa kwa watoto, kuna changamoto kubwa hasa vijijini ya watoto ambao wameathirika na utapiamlo na kwashakoo. Hivyo serikali haina budi kuwekeza hela katika kuhakikisha lishe bora kwa watoto


**Kielelezo Na 7.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 7

Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeandika insha kuhusu ‘‘*Umuhimu wa lishe bora kwa watoto*’’ kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa insha na kutoa hoja madhubuti za umuhimu wa lishe bora kwa watoto.

Aidha, watahiniwa 164,186 sawa na asilimia 31.11 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani wa alama kati ya 3 na 5.5. Watahiniwa hao waliweza kuandika insha kwa kuzingatia baadhi ya taratibu za uandishi na

kushindwa kukidhi taratibu zingine za uandishi wa insha kuhusu "*Umuhimu wa lishe bora kwa watoto*." Baadhi yao waliandika insha yenye hoja zisizojitosheleza na wengine walishindwa kuandika utangulizi au hitimisho zuri linaloendana na insha husika. Aidha, wapo watahiniwa walioandika insha bila kuzingatia alama za uandishi na idadi stahiki ya maneno waliyopewa (200 hadi 250), hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 69,454 sawa na asilimia 13.12 walikuwa na ufaulu hafifu kutokana na kukosa maarifa ya kutosha ya uandishi wa insha, hivyo kupata alama kati ya 0 na 2.5. Watahiniwa hao walishindwa kuandika insha yenye maneno mia mbili (200) hadi mia mbili na hamsini (250) kuhusu ‘‘*Umuhimu wa lishe bora kwa watoto*” Baadhi yao, waliandika insha isiyozingatia vigezo muhimu kama vile kutumia lugha fasaha na sanifu, kuwa na mtiririko na ushikamani wa mawazo, matumizi sahihi ya alama za uandishi, na idadi stahiki ya maneno. Wengine waliandika insha bila kuzingatia kiini cha insha. Pia, wapo walioandika insha zenye sentensi ndefu zisizo na kituo wala mkato. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika insha kuhusu UKIMWI kinyume kabisa na matakwa ya swali hili na kupata 0. Mtahiniwa mwingine aliandika insha yenye aya moja pekee bila utangulizi wala hitimisho, hivyo kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili na kupata alama hafifu.



7. UMUHIMU WA LISHE BORA KWA WATOTO

Lishe huwa na maana kamili inaochangia katika majenikio ya jamii nzima. Lishe imejaribu kuchangia maendeleo katika nchi za nje na ndani. Yafuatayo ni umuhimu wa lishe bora kwa watoto.

Inachangia kuleta itamaduni bora katika jamii. Hii ni mmoja wapo umuhimu wa lishe katika jamii, kwa inajenisha adhabu kwa watoto ili kuleta uheshima, majenikio na upendo katika baina ya wao.

Huchangia kupunguza umaskini kwa watoto. Hii pia mmoja wapo umuhimu wa lishe katika jamii. Kwa sababu lishe huweza kutoa jonzo kwa kuwa mambo ya kuzingatia ili kuhakikisha majenikio katika jamii.

Huelimisha watoto katika baina ya wao. Hii pia ni mmoja wapo umuhimu wa lishe katika jamii, kwa sababu inachangia katika ujuzi wa vitu tofauti mfano sayansi na teknolojia, biashara na mengineyo katika dunia.

Hujengea hekima na uhirikiano kwa watoto. Hii pia ni moja wapo umuhimu wa lishe kwa watoto katika jamii. Kwa sababu lishe inachangia katika kupata majenikio na ujuzi katika umuhimu na faida za uhirikiano kwa inachangia katika kupata mambo mengi.

Huchangia kuepusha matendo mabaya katika jamii. Hii pia moja wapo faida za lishe katika baina ya watoto. Kwa sababu hii inasaidia sana watoto watoto wapate ujuzi kwa mambo mabaya pia yanamadhara mabovu katika jamii yetu kujika. Mfano umalaya unaleta usambazaji wa UKIMWI katika jamii yetu.

Kwa kuhitimiza lishe ina umuhimu wake kama ikiwa ndhibitishwa ndo maana ni muhimu serikali ichangia katika swala hii kwa watoto tofauti tofauti duniani.

**Kielelezo Na. 7.2:** Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 7

Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeandika insha kwa kutoa hoja zisizohusiana na kichwa cha insha "*Umuhimu wa lishe bora kwa watoto*" japokuwa aliweza kuandika kichwa cha insha kwa herufi kubwa. Hata hivyo, utangulizi na hitimisho lake halikukidhi matakwa ya swali, hivyo kupata alama hafifu.

### 2.2.6 Swali la 8: Ufahamu

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ufahamu*, hususani mada ndogo ya *Ufahamu wa Kusoma Kifungu cha Habari* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa kuelewa kifungu cha habari. Swali lilimtaka mtahiniwa kusoma kifungu cha habari kisha kujibu maswali yaliyofuata. Kifuatacho ni kifungu cha habari walichopewa.

*Mchezo wa jana wa mpira wa miguu ulikuwa patashika nguo kuchanika. Katika kutupia macho wachezaji wa Tunisia, ni dhahiri kuwa mtazamaji yeyote angeweza kutabiri kuwa wachezaji gani wangejipatia ushindi. Wachezaji wa Tunisia walionekana kuwa majitu ya miraba minne na hivyo kutabiriwa kuwa washindi wa mchezo huo.*

*Kwa siku za nyuma, wachezaji wa timu ya Tanzania wawaliweza kwenda sare na timu ya Tunisia kwa kipindi chote cha mchezo na pengine hawakuweza kupata ushindi kabisa. Kutokana na hilo, hofu kubwa ilitanda miongoni mwa Watanzania kwani siku hiyo huenda historia ikajirudia ya kufungwa au kutoka sare. Kipenga kilipolia wachezaji wa pande zote mbili walijitupa uwanjani wakionesha utanashati na manjonjo mengi huku wakipiga mazoezi ya hapa na pale. Watu walipowashangilia kwa hoi hoi na vifijo waliongeza madaha yao. Haukupita muda mrefu walitengana na kila mmoja alikwenda sehemu yake na mara kipenga cha kuashiria mpira kuanza kikapigwa. Naam, ilianza vuta nikuvute, kila mmoja akiwania kuanza kuufumania mlango wa mpinzani wake. Kukuru kakara hiyo iliendelea hadi mwisho wa kipindi cha kwanza ambapo hakuna aliyefanikiwa kugusa nyavu za mwenzie. Kwa kipindi hiki chote timu ya Tanzania ilionekana kupiga moyo konde na kuwania ushindi. Wachezaji wa Tunisia nao waliapa kutoshindwa kuwatoa Watanzania kama walivyotazamia.*

*Kipindi cha pili kilianza kwa kila mchezaji kujihami dhidi ya adui yake ili mradi kila mmoja apate nafasi ya kuutundika mpira wavuni. Hata hivyo wachezaji wengi wa pande zote walionekana kulowa kwa kutoelewa nini kitatokea mbele yao baada ya dakika arobaini na tano zilizofuatia.*

*Muda mfupi baada ya kipindi cha pili kuanza, timu ya Tunisia iliona lango la timu ya Tanzania na kujiandikia bao la kwanza. Uwanja mzima ulipooza kwa upande wa Watanzania lakini Watunisia walionekana kufunguka nyuso zao kwa bashasha. Waswahili wanasema, "Mungu si Athumani." Hivyo, ilipotimia dakika ya themanini ya mchezo, Mohamedi Kajole alipata nafasi nzuri, akautoma mkwaju mkali kinywani mwa lango la Tunisia na kuiandikia timu ya Tanzania goli la kusawazisha. Nderemo, shangwe, vifijo na vigelegele vilitawala uwanjani kwa kuwa Kajole aliwatoa Watanzania aibu katika kiwanja cha nyumbani.*

*Mchezo ulikuwa kama umepata mvuto na ari mpya kwa wachezaji wa Tanzania ambao walionekana kuwa na kasi kubwa katika kupasiana mpira. Wachezaji wa Tunisia walianza kuhangaika uwanjani wakijua kuwa ushindi karibu utatoweka mikononi mwao. Mashabiki wa Tanzania nao walishika kasi katika kushangilia timu yao.*

*Harakati hizo zilizaa matunda katika dakika ya thamanini na tisa pale Kasimu Kapombe alipoipatia timu yake ya Tanzania goli la ushindi. Vifijol hoi hoi na shangwe zilitawala uwanjani kwa upande wa Watanzania. Lakini mambo hayakuwa mazuri kwa upande wa timu ya Tunisia kwani walichokitegemea hawakukipata. Hadi mwisho wa mchezo huu, Tanzania iliibuka kidedea kwa mabao mawili dhidi ya bao moja la Tunisia.*

Watahiniwa 529.437 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri, ambapo watahiniwa 474,475 sawa na asilimia 89.62 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Aidha, watahiniwa 54,962 sawa na asilimia 10.38 walikuwa na ufaulu hafifu. Jedwali Na. 3 linaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kiasilimia.

**Jedwali Na. 3: Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa**

| Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0.0 - 2.5 | 54,962 | 10.38 |
| 3.0 - 5.5 | 204,567 | 38.64 |
| 6.0 - 9.0 | 269,908 | 50.98 |

Jedwali Na. 3 linaonesha kuwa, watahiniwa 269,908 sawa na asilimia 50.98 walifaulu kwa kiwango kizuri cha alama 6 – 9; watahiniwa 204,567 (38.64%) walifaulu kwa kiwango cha wastani cha alama 3 – 5.5; na watahiniwa 54,962 (10.38%) walifaulu kwa kiwango hafifu cha alama 0 – 2.5.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa zaidi ya nusu ya watahiniwa (269,908) sawa na asilimia 50.98 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa juu kwa kupata alama kati ya 6 na 9. Ufaulu mzuri ulitokana na watahiniwa wengi kuwa na umahiri wa kutosha wa kusoma kifungu cha habari na kujibu kwa usahihi maswali yaliyotokana na habari husika. Watahiniwa hao katika kipengele (a) walipendekeza kwa usahihi kichwa cha habari yaani MECHI KATI YA TANZANIA NA TUNISIA; (b) walieleza kwa usahihi mawazo waliyokuwa nayo watazamaji wengi kabla ya kuanza mpira kuwa *walijenga Imani kubwa kwa timu ya Tunisia kupata ushindi kutokana na wachezaji wake kuonekana kuwa na nguvu nyingi na kujiamini sana*; (c) walieleza kwa usahihi maana ya misemo kama ilivyotumika katika kifungu cha habari walichopewa kama vile: (i) *Patashika nguo kuchanika* kuwa ni kazi nzito iliyohitaji jitihada kubwa na kujituma; (ii) *Walipiga moyo konde* kuwa ni kujipa moyo; (iii) *Mungu si Athumani* kuwa Mungu hana upendeleo; (iv) *Waliibuka kidedea* kuwa walipata ushindi; na (v) *Walishika kasi* kuwa ni *Kuongeza nguvu*. Aidha,

katika kipengele (d), walieleza kwa usahihi hali waliyokuwa nayo Watunisia baada ya kufungwa goli la pili kuwa *walinyong'onyea na kushikwa na huzuni*; na (e) walifupisha habari waliyopewa kwa usahihi wakizingatia vigezo vya uandishi wa ufupisho kama vile: *kusadifu mawazo makuu*, *kuzingatia alama za uandishi*, *kuzingatia idadi ya maneno* (100 – 105), *kutumia lugha sanifu*, na *kutopotosha kiini cha habari waliyosoma*. Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama zote.

8a) MCHEZO WA TUNISIA NA TANZANIA

b) Watazamaji wengi walikuwa na mawazo kwamba Tunisia wangeibuka washindi wa mchezo huo kwani walionekana kuwa watu wakubwa.

c) i) Patashika nguo kuchanika
Inamaanisha ushindani mkubwa.

ii) Walipiga moyo konde.
- Walijipa moyo kuwa watashinda.

iii) Mungu si Athumani
- Bahati za mwenyezi Mungu (Mungu sio kama binadamu yeye ana uwezo mkubwa)

iv) Waliibuka kidedea.
- Waliibuka washindi katika mashindano yao.

v) Walishika kasi.
- walikuwa na haraka katika kupasiana magoli ili waweze kuibuka washindi.

d) Watunisia walijisikia vibaya kufungwa goli la pili kwani waliyotegemea hawakukupata.

8e.
Ilikuwa siku nzuri wachezaji toka Tunisia waliwasili Tanzania ili kuweza kucheza mpira wa miguu wao dhidi ya Watanzania. Ilikuwa ni siku ya moto

8e) sana kwani kila timu ilihitaji ushindi kwa siku ile
Wachezaji toka Tunisia walionekana kuwa ma
jitu hata kuleta hofu kwa wachezaji wa Tanzania na
kufanya wadhani kuwa wangefungwa siku hiyo na
watunisia.
Wakati mchezo unaendelea wachezaji wote wali
onekana kuwa mahiri kwani wote walitumia vizuri
uwanja hivyo kila watu walikuwa wakiwashangilia
watu wao kwani wote walihitaji ushindi.
Kadri mchezo ulivyoendelea Tunisia wakafunga
bao moja. Watanzania waliogopa japo wachezaji wao
walizidi kupambana. Kwa kudra za Mungu Tanzania
na walifunga goli. cha kufurahisha zaidi wakaongezea la
pili.
Siku hiyo Tanzania wakaibuka washindi dhi
di ya Tunisia kwa bao mbili kwa moja.


**Kielelezo Na. 8.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 8

Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha kuwa, mtahiniwa alikuwa na uelewa wa kutosha wa maudhui yaliyomo katika kifungu cha habari, hivyo kujibu kwa usahihi vipengele (a) na (b) na kupata alama za juu.

Aidha, watahiniwa 204,567 sawa na asilimia 38.64 waliofanya swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani. Hali hii ilitokana na kujibu kwa usahihi baadhi ya maswali yaliyotokana na habari waliyopewa na kushindwa kufanya hivyo kwa baadhi ya maswali katika vipengele vingine. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walipendekeza kichwa sahihi cha habari katika kipengele (a), na katika kipengele (b) walielezea kwa usahihi mawazo waliyokuwa nayo watazamaji kabla ya kuanza mpira. Vilevile, katika kipengele (d) walielezea kwa usahihi hali waliyokuwa nayo Watunisia baada ya kufungwa goli la pili. Hata hivyo, katika kipengele (c)

walishindwa kuandika maana sahihi za maneno yote waliyopewa kama yalivyotumika katika habari; na katika kipengele (e) baadhi walishindwa kufupisha habari kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa ufupisho, hivyo kupata alama za wastani 3 hadi 5.5.

Hata hivyo, watahiniwa 54,962 sawa na asilimia 10.38 walijibu vibaya swali hili na kupata alama kati ya 0 na 2.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kukosa umahiri wa kujibu maswali yatokanayo na kifungu cha habari. Watahiniwa hao walishindwa pia kufupisha habari kwa maneno yasiyopungua mia moja (100) na yasiyozidi mia moja na tano (105). Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kipengele (a) alipendekeza kichwa cha habari kisichohusiana na habari aliyoisoma kwa kuandika KILIMO CHA MPIRA TUNISIA badala ya MECHI KATI YA TANZANIA NA TUNISIA. Katika kipengele (b) alishindwa kuelezea mawazo waliyokuwa nayo watazamaji kabla ya kuanza kwa mpira kwa kuandika *Watunisia hawajui mpira* badala ya ushindi uliotarajiwa na watazamaji kwa uzuri wa timu ya Tunisia. Katika kipengele (c) aliandika maana zisizo sahihi kama vile: (i) **Patashika nguo kuchanika** kuwa ni *kutupia macho wachezaji wa Tunisia,* (ii) **Walipiga moyo konde** – *kiapo cha wachezaji wa Tunisia,* (iii) **Mungu si Athumani** - *dakika ya themanini ya mchezo ilipotimia,* (iv) **Waliibuka kidedea** – *kushangilia timu yao*, na (v) **Walishika kasi** - *walizomeana.* Kadhalika, katika kipengele (d) alishindwa kuelezea kwa usahihi hali waliyokuwa nayo Watunisia baada ya kufungwa goli la pili kwa kuandika *hali timilifu*; Aidha, katika kipengele (e) aliandika ufupisho usiokuwa na ushikamani hivyo kutokuwa na mantiki; usiozingatia ukomo wa idadi ya maneno (100 – 105), kutotumia maneno yake mwenyewe na kutumia sentensi ndefu zisizo na mkato wala nukta. Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vipengele vyote vya swali hili na kupata 0.


8. a) Mpira wa miguu

b) Nidhahiri kuwa mtazamaji yeyote ange weza kutabiri kuwa wacherazji gani wange jipatia ushidi

c) i) Ana maanisha kuwa mcherouli kuwa wa ushidani

ii) Ana maanisha kuwa kuvumilia kwajambo furani

iii) Ananaanisha kuwa Mungu hamtupi mjawake

iv) Kushinda jambo

v. walishambulia kwanguvu

d. i) Walianza kuhangaika uwanjani wakijua kuwa ushindi karibu utatoweka mikononi mwao

e) MCHEZO KATI YA TANZANIA NA TUNISIA BAADA YA TANZANIA KUMFUNGA TUNISIA GOLI MBILI KWA MOJA TUNISIA HAKUAMINI HADI MCHEZO UKAISHA TANZANIA AKIONGOZA

**Kielelezo Na. 8.2**: Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 8

Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali kwa sehemu kubwa na kujibu kwa usahihi kipengele (c) (ii), (iii), na (v) na kipengele (d). Vilevile, alishindwa kujibu kwa usahihi vipengele (a), (b), (c) (i) na (iv) na (e) na kupata alama hafifu.


## 2.3 SEHEMU C: MASWALI YA MAJIBU MAREFU

Sehemu C ilikuwa na maswali matatu na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili (2) tu na swali la tisa (9) lilikuwa la lazima. Sehemu hii ililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kuchambua na kutathmini kazi za fasihi andishi. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 30, ambapo kila swali lilikuwa na alama 15.

### 2.3.1 Swali la 9: Uhakiki wa Ushairi

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutathmini matumizi ya lugha katika diwani teule. Swali lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha ukweli wa kauli, "lugha ni nyenzo muhimu katika kutoa mafunzo kwa jamii" kwa kutumia vipengele vitatu vya lugha kwa kila kitabu kutoka katika diwani mbili walizosoma.

Watahiniwa 529,437 sawa na asilimia 100 ya waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani ambapo watahiniwa 222,528 sawa na asilimia 42.03 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Aidha, watahiniwa 306,909 sawa na asilimia 57.97 walikuwa na ufaulu hafifu. Chati Na. 7 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na.7:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 9*

Chati Na. 7 inaonesha kuwa, watahiniwa 75,936 sawa na asilimia 14.34 walifaulu kwa kiwango kizuri cha alama 10 – 15; watahiniwa 146,592 (27.69%) walifaulu kwa kiwango cha wastani cha alama 4.5 – 9.5; na watahiniwa 306,909 (57.97%) walifaulu kwa kiwango hafifu cha alama 0 – 4.

Kutokana na swali hili kuwa na ufaulu wa wastani, watahiniwa 306,909 sawa na asilimia 57.97 walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama kati ya 0 na 4. Kati yao, watahiniwa 123,328 sawa na asilimia 23.29 walipata alama 0 kutokana na kukosa umahiri kuhusu kipengele cha lugha katika ushairi kinavyoweza kuwa nyenzo muhimu katika kutoa mafunzo kwa jamii. Watahiniwa wengi walioshindwa kujibu swali hili walionesha kutokuwa na uelewa wa vipengele vya lugha vinavyotumika katika diwani teule ambapo baadhi walithibitisha kauli inayosema, "*Lugha ni nyenzo muhimu katika kutoa mafunzo kwa jamii"* kwa kutumia dhamira mbalimbali zilizojitokeza katika diwani walizosoma.

Watahiniwa wengine walijadili vipengele vya fani kama vile *muundo, mtindo, mandhari* na *wahusika* kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alithibitisha kauli hiyo kwa kujadili *wasifu wa wahusika* katika diwani ya "Malenga Wapya" na "Wasakatonge" na mwingine alijadili dhamira za *matabaka, wizi na uongozi mbaya* katika diwani hizo kinyume na matakwa ya swali. Watahiniwa hao walitakiwa kutumia kipengele kimoja tu cha fani ambacho ni *lugha* ili kuthibitisha ukweli wa kauli waliyopewa kwa kuangalia matumizi ya tamathali za semi, taswira, misemo, methali na nahau. Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili na kupata 0.


09. Dhamira; ni kazi ya fasihi inayo wasilishwa na Msanii kufika au kwenda katika jamii kwa kutoa mapenzo kwa jamii. Kupitia Diwani mbili nazo ni Diwani WASAKATONGE Mwandishi ni M. Sikhatibu na Diwani MALENGA WAPYA Mwandishi ni TAKILUKI kuna dhamira zipeatazo mbalimbali na Mapenzo yake. Kwa kuanza na Diwani WASAKATONGE Mwandishi ni M. S. khatibu kuna dhamira na Mapenzo yake kama zipeatazo;

Kupiga vita Umasiki; Mwandishi akionyesha jamii yetu imekumbwa na wimbi kubwa la Umasiki. Dhamira hii inatupa ujumbe kwa Umasikini hupelekea watu kupoteza Maisha yao kwa ukosefu wa Mahitajio yao Muhimu. Imeonyeshwa katika Shairi la WASAKATONGE uk-05. katika shairi Anasema;

"Jua kali na wasakatonge"
Waoni Manamba Mashambani, ni wach
ni wachapakazi viwandani,
ni Mayaya na Madobi wa Nyumbani
ni Matopasi Majaani
Lakini Bado Masikini.

Kwenye jamii yetu Umasikini bado upo ambapo hupelekea athari mbalimbali kwa watu.

Kupiga Vita ukoloni Mamboleo; Mwandi


9. ameonyesha katika shairi la KOSA uk-3, Mwandishi akisema, hali hii kuringinia nchi kujiamulia au kujipa uhuru wao kwa kutawaliwa na Nchi nyingine kimabavu. dhamira hii inatupa ujumbe kwa Ukoloni-Mamboleo ni chanzo cha nchi kutokua na Maendeleo. katika shairi Anasema.

Mmetupunga kama,
za Miguuni,
za Mikononini,
za Mdomoni,
na Mkatutosa baharini.

kwenye jamii zetu bado ukoloni mamboleo upo na hali hiyo kuringinia uhuru jamii au nchi kujiamulia au kujipa uhuru wake.

Kupiga Vita Usaliti; Mwandishi-anasema Usaliti umejitokeza kwa Viongozi wetu kwani Mapanikio yakipatikana huwatenga wananchi wao. Dhamira hii inatupa Ujumbe kwa ni muhimu kupiga vita Usaliti. katika shairi la KINYONGA uk-49. katika shairi Anasema.

Tukiwaani,
Mmeingilia,
Wananasa Vinyonga,
Kauli zao Nzuri,
Maisha ya ufahari,
Matendo yao hatari,
Ni kinyume na Maadili,
ni Usaliti

kwenye jamii yetu hii ya leo pia katika nchi yetu kuna unafiki wa Viongozi pale ambapo wanapata Mapanikio wanawatenga wananchi wao.

**Kielelezo Na. 9.1:** Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 9

Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejadili dhamira mbalimbali zilizojitokeza katika diwani ya "Wasakatonge" Pia, katika utangulizi wake alitoa maana ya dhamira kinyume na matakwa ya swali, hivyo kupata 0.

Watahiniwa 146,592 sawa na asilimia 27.69 waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kati ya 4.5 na 9.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuthibitisha kauli "*Lugha ni nyenzo muhimu*

*katika kutoa mafunzo kwa jamii"* kwa kutumia diwani moja au kutoa hoja zisizojitosheleza au zinazojirudiarudia. Aidha, baadhi yao walitumia kipengele kimoja au viwili vya lugha kutoka katika diwani moja na wengine walitumia kipengele kimoja tu cha lugha katika diwani zote. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia tamathali za semi pekee katika vitabu vyote badala ya kutumia vipengele vitatu vya lugha kwa kila diwani kama ilivyotakiwa, hivyo kupata alama za wastani.


Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 75,936 sawa na asilimia 14.34 walifanya vizuri swali hili na kupata alama za juu kati ya 10 na 15. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kuonesha umahiri mkubwa wa uhakiki wa ushairi. Watahiniwa hao walitumia vipengele vitatu vya lugha kutoka katika kila diwani ili kuthibitisha kauli kuwa "*Lugha ni nyenzo muhimu katika kutoa mafunzo kwa jamii."* Mathalani, mtahiniwa mmoja katika diwani ya **Wasakatonge** alitumia vipengele vitatu vya lugha ambavyo ni *tashihisi* (tamathali za semi), *nahau* (semi), na matumizi ya *taswira*. Vivyo hivyo katika diwani ya **Mashairi ya Chekacheka** alitumia *misemo*, *matumizi ya sitiari*, na *tabaini* huku akitoa mifano sahihi ya mashairi ili kuthibitisha kauli hiyo. Kadhalika, Katika diwani ya **Malenga Wapya,** mtahiniwa mwingine alitumia kwa usahihi vipengele vya *taswira*, *nahau* na *misemo* na kupata alama za juu. Kwa ujumla, watahiniwa hao waliandika utangulizi na hitimisho sahihi lililoendana na swali hivyo kukidhi matakwa ya swali hili. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili.

9 Lugha. ni jumla ya mambo yote yatumikayo katika mawasiliano ya kila siku ya jamii husika. Na ni nyenzo muhimu katika kutoa mafunzo kwa jamii. Nathibitisha kauli hii kwa kutumia diwani mbili ya WASAKATONGE iliyoandikwa na MOHAMED SEIF KHATIBU na diwani ya MALENGA WAPYA iliyoandikwa na TAKILUKI. Kwa kuanza na diwani ya WASAKATONGE iliyoandikwa na MOHAMED SEIF KHATIBU yafuatayo ni matumizi ya lugha katika kutoa mafunzo.

Taswira. ni lugha ya picha, hutumia neno dogo kuwakilisha kitu fulani mfano taswira ya "Nahodha" kama ilivyotumika katika shairi la "Nahodha" ikiwa na maana ya viongozi wanaong'ang'ania madaraka licha ya kushindwa kuongoza. Taswira hii inatufunzo sisi kama wanajamii kuchagua viongozi wazuri ambao wataongoza jamii kwa haki bila ya kuacha kuwajibika kama wanavyoahidi muda wa kampeni.

Tashibiha. Tamathali ya semi yenye kutumia viunganishi kuonesha ulinganishi mfano "Ianuka kama ng'onda" kama ilivyotumika katika shairi la "kansa" kuonesha kuwa jamii imeoza na inanuka kama ng'onda. watu wana tabia chafu na viongozi hawawajibiki. Funzo hapa ni kuacha anasa za dunia watu wote ikiwamo viongozi ili kuleta maendeleo katika jamii tunazoishi wenyewe

Majumbo. lugha ya upicha pia mwandishi ametumia lugha hii kupicha maana ya neno fulani mfano "wewe jiko la shamba" katika shairi la wewe jiko la shamba mwandishi ametumia jumbo hili kuonesha au kuwa na maana ya umalaya, ambao upo katika jamii zetu. Funzo hapa ni kuacha na kupinga mmomonyoko wa maadili. katika jamii zetu kwani ni chanzo cha maendeleo duni na magonjwa katika jamii. Kwa kutumia diwani ya MALENGA WAPYA iliyoandikwa na TAKILUKI waandishi wametumia lugha kutoa mafunzo yafuatayo.



9 Methali. Waandishi wametumia kipengele hiki cha lugha kutoa funzo kwa jamii. Methali iliyotumika ni "Subira yavuta kheri" katika shairi la "Usiharakie maisha". Inatuasa kufanya mambo kwa muda muafaka na kutokukimbilia mbele kwani subira yavuta kheri hivyo tunapaswa kwenda kwa hatua na hatimaye tutafanikiwa zaidi.

Taswira. Waandishi hawa pia wametumia lugha ya picha mfano "Ua" kuonesha msichana mrembo. Na mtunzi wa shairi anasifia uzuri wa mwenzi wake aliyonao. Funzo ni kwamba vijana na watu wote wanaooa au kuolewa wanapaswa kuchagua watu wazuri yaani kitabia na kimatendo na kutokuangalia mazuri aliyonayo.

Tashihisi. Tamathali ya semi inayohusisha kuvipa viumbe hai uwezo wa kutenda kama binadamu. Katika shairi la "Samaki mtungoni". "Samaki" wamepewa uwezo wa kibinadamu wa kupambania haki zao. Shairi hili na lugha hii inatoa funzo kwamba tuache matabaka tuungane pamoja ili kufanikisha na kuleta maendeleo katika jamii.

Hivyo, lugha itumikayo katika diwani hutoa mafunzo mema ya kimaadili. Hivyo watu wanashauriwa kusoma vitabu hivi vya ushairi vizuri na kuvielewa kwa upana kwani hubeba ujumbe na mafunzo mazuri kwa jamii zetu za sasa. Ili tuweze kuepusha matatizo katika jamii na kuhimiza maendeleo zaidi.


**Kielelezo Na. 9.2:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 9

Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi swali hili kwa kutumia *tashibiha, mafumbo, taswira* na *tashihisi* kutoka katika diwani ya “Wasakatonge” na “Malenga Wapya” na kuthibitisha namna vilivyotumika kama nyenzo muhimu katika kutoa mafunzo kwa jamii, hivyo kukidhi ipasavyo matakwa ya swali hili na kupata alama za juu.

### 2.3.2 Swali la 10: Uhakiki wa Riwaya

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi* hususani mada ndogo ya *Uhakiki wa Riwaya* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kuchambua na kutathmini kazi mbalimbali za kifasihi hususani riwaya. Swali lilimtaka mtahiniwa kuchagua mhusika mmoja kwa kila kitabu kisha kuonesha namna kila mmoja alivyowasilisha mawazo matatu ya mwandishi kutoka katika riwaya mbili alizosoma.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 298,684 sawa na asilimia 56.42 ya waliofanya mtihani kwa kuwa lililkuwa la kuchagua. Swali lilikuwa na ufaulu mzuri ambapo watahiniwa 263,643 sawa na asilimia 88.27 walifaulu kwa kiwango kizuri, na cha wastani. Kwa upande mwingine, watahiniwa 35,041 sawa na asilimia 11.73 walikuwa na ufaulu hafifu. Chati Na. 8 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 10*

Chati Na. 8 inaonesha kuwa, watahiniwa 216,258 sawa na asilimia 72.41 walifaulu kwa kiwango kizuri cha alama 10 – 15; watahiniwa 47,385 (15.86%) walifaulu kwa kiwango cha wastani cha alama 4.5 – 9.5; na watahiniwa 35,041 (11.73%) walifaulu kwa kiwango hafifu cha alama 0 – 4.

Aidha, watahiniwa 216,258 sawa na asilimia 72.41 walifanya vizuri swali hili na kupata alama za juu kati ya 10 hadi 15. Watahinwa hao walionesha

umahiri wa kutosha wa kuhakiki riwaya teule, hivyo kuchagua kwa usahihi mhusika mmoja kwa kila kitabu na kuonesha namna kila mmoja alivyowasilisha mawazo matatu ya mwandishi kutoka katika riwaya mbili alizosoma. Kati yao, asilimia 28.49 walipata alama za juu (14 hadi 15) kwa kuwa waliweza kutoa hoja sahihi tatu kwa kila riwaya katika kuonesha namna kila mhusika alivyowasilisha mawazo matatu ya mwandishi kutoka katika riwaya mbili alizosoma. Kwa mfano, katika riwaya ya "Watoto wa Mama N'tilie" mtahiniwa mmoja alimwonesha mhusika *Mzee Lomolomo* alivyowasilisha mawazo matatu ya mwandishi kama vile: *ulevi*, *kutowajibika katika familia*, na *mapenzi ya uongo* na katika riwaya ya "Takadini" alimtumia mhusika *Sekai* kuwasilisha mawazo ya mwandishi kama vile *ujasiri*, *mchapakazi*, na *mwenye upendo wa dhati*. Mtahiniwa huyu alifafanua kwa usahihi namna wahusika hao walivyowasilisha mawazo ya waandishi katika kazi ya fasihi. Kwa ujumla, watahiniwa hao walitoa hoja zikiambatana na mifano sahihi kutoka kwenye riwaya hizo ili kuthibitisha mawazo ya waandishi husika. Aidha, waliandika utangulizi mzuri wenye ufafanuzi sahihi kuhusu wahusika na jinsi walivyotumiwa na waandishi ili kuwasilisha mawazo yao kwa jamii. Pia, waliweza kuandika hitimisho zuri lililokidhi matakwa ya swali. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

10. Mhusika ni kitu kinachotumiwa na mtunzi wa
fasihi kuwasilisha mawazo yake katika kazi yake. kwa
kutumia Riwaya ya JOKA LA MDIMU iliyoandikwa na A.J.
Safari pamoja na riwaya ya WATOTO WA MAMA N'TILIE
iliyoandikwa na. Emmanuel Mbogo.
Kwa kutumia riwaya ya JOKA LA MDIMU. afuatayo ni
Mhusika anayebeba mawazo ya mwandishi ambaye ni Brown
Kwacha.
Brown kwacha ni malaya ; malaya ni mtu
anayeshiriki tendo la ndoa na waenzi zaidi ya mmoja. tunao
na kuwa Brown kwacha anamuacha mke wake na kufanya
mapenzi na wasichana wengine kama Josephine na leila. mwandishi
kamtumia Brown kwacha kufikisha wazo la Umalaya katika Jamii
. hata kwenye jamii zetu umalaya unafanyika na watu kama
Brown Kwacha.
Brown kwacha ni kiongozi mbaya ; Tunamuo
na Brown kwacha akichoma ofisi yake kutaka kufuta ushahidi
wa ~~katika~~ anayoyatenda baada ya kuombwa nyaraka zake na
serikali. Mwandishi anamtumia Brown kwacha kuwasilisha wazo
la Uongozi mbaya. hata kwenye jamii zetu kuna viongozi kama

Brown Kwacha.

Brown Kwacha ni jangili; jangili ni mtu anayeuwa nyama poli. tunamuona Brown Kwacha anafanya kazi ya ujangili pamoja na kusafirisha pembe za ndovu pamoja na kifaru nchi za nje. Mwandishi anamtumia Brown Kwacha kuwasilisha wazo la ujangili katika jamii. hata kwenye jamii zetu wapo watu kama Brown Kwacha wenye tabia kama zake.

Kwa kutumia riwaya ya KIVATOTO WA MAMA NTILIE afuataye ni mhusika Mama Ntilie anayowasilisha mawazo ya mwandishi

Mama Ntilie anamapenzi ya dhati; Tunamuona Mama ntilie anakuwa na mapenzi ya dhati kwa mumewe Mzee lomolomo licha ya ulevi wake kumsumbua kumtelekeza. mwandishi anaibua wazo la Mapenzi na ndoa katika jamii. hata kwenye jamii wapo wanawake kama Mama ntilie.

Mama ntilie ni mlezi wa familia; Tunamuona Mama ntilie analea familia yake kwa kuihudumia chakula kwa kazi kidogo cha pesa anachopata pia anapigana ili wanae waende shule. Mwandishi anaibua wazo la Malezi kama wazo. hata katika jamii zetu kuna wanawake kama Mama ntilie.

Mama ntilie ni mchapakazi; Tunamuona mama ntilie anajitahidi kutimiza kazi yake kama mama wa familia kwa kuuza chakula katika kibanda chake na kuletea watoto na mzee lomolomo chakula nyumbani. Mwandishi anaibua wazo la uwajibikaji na uchapakazi. hata kwenye jamii zetu wapo wanawake kama Mama ntilie kwa uchapakazi wao.

Hivyo basi; Mwandishi hawezi kufikisha vyema kazi ya fasihi bila kutumia wahusika ili kuwasilisha mawazo yake. kwa mantiki hiyo mhusika ni muhimu katika kazi ya fasihi katika jamii.

**Kielelezo Na. 10.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 10

Kielelezo Na. 10.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kuwatumia wahusika *Mama N'tilie* na *Brown Kwacha* ambao walitumiwa na waandishi wa riwaya za "Mama N'tilie" na "Joka la Mdimu" ili kuwasilisha mawazo yao.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 47,385 sawa na asilimia 15.86 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani kwa kupata alama kati ya 4.5 na 9.5. Watahiniwa hao walichagua mhusika mmoja kwa kila riwaya lakini walimudu kuonesha wazo moja au mawili yaliyowasilishwa na wahusika badala ya mawazo matatu kama swali lilivyotaka hivyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa watahiniwa 35,041 sawa na asilimia 11.73 waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama kati ya 0 na 4. Watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kuhakiki kazi za fasihi andishi hususani riwaya. Watahiniwa hao walikosa uelewa wa riwaya teule, hivyo kushindwa kubaini wahusika katika riwaya hizo na kuonesha namna kila mmoja anavyowasilisha mawazo matatu ya mwandishi kinyume na matakwa ya swali. Aidha, baadhi yao walichambua dhamira mbalimbali zilizomo katika riwaya hizo na wengine waliorodhesha wahusika katika riwaya na kueleza wasifu wao kinyume na matakwa ya swali. Pia, wapo watahiniwa waliochanganya mawazo ya wahusika wa riwaya moja na nyingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichagua wahusika watatu kwa kila riwaya ambapo katika riwaya ya "Takadini" aliwatumia wahusika *Takadini*, *Sekai*, na *Shangai*. Kadhalika katika riwaya ya "Watoto wa Mama Ntilie" aliwatumia wahusika *Mama Ntilie*, *Lomolomo*, na *Zenabu* badala ya kuchagua mhusika mmoja kwa kila riwaya kisha kuonesha namna walivyowasilisha mawazo matatu ya waandishi wa riwaya hizo. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili na kupata alama hafifu.

10 Fasihi ni ni jumla ya vipengele vyote vya fani na maudhui ambavyo hutoa ujumbe kwa hadhira. Mhusika wa fasihi hawezi kuwa kamili kwani kila kitu sio kikamilifu. kwa kutumia riwaya ya "TAKADINI" iliyoandikwa na "BEN J. HANSON" pamoja na watoto wa mama ntilie "WATOTO WA MAMA NTILIE" kilicho andikwa na "EMMANUEL MBOGO" wamoweza kufaulu hata kufeli katika kuwasilisha kazi zao za sanaa kwa kuanza na "TAKADINI" amefeli katika uwasilishaji wa kazi yake fasihi kwa hadhira

Amefeli kuonesha matatizo ya ndoa za mitala. Mzee makwati alikua na wake wengi ambao ndio chanzo cha umasikini wake. lakini mwandishi ameshindwa kuonesha ni kwa namna gani makwati alikua maskini na jinsi gani ambavyo hakuweza kutatua shida yake ya umaskini.

Amefeli kuonesha athari ya kukosa Elimu juu ya sope. katika kitabu hiki ameonesha kuwa sope alizaliwa na kila mtu alitaka kumuua kwa alikua ni tofauti na wao. lakini mwandishi ameshindwa kutuonesha ni kwa namna gani Elimu inabidi itolewe kwa hao wanakijiji yupo sope. kwani hata masope huweza kushiriki katika kukuza uchumi wa nchi, Hivyo basi inatupasa kuto wanyanyapaa watu wenye ulemavu kwani hata wao ni kama sisi.

10 Amefeli kuonesha suluhisho la ugomvi kati ya Nhamo na Takadini. Mwandishi wa kitabu ameonesha tu chanzo cha ugomvi kla takadini na nhamo kuwa shingai alimpenda takadini kuliko Nhamo hivyo ameshindwa kuonesha suluhisho la ugomvi klao.
Pia kitabu cha "KlATOTO KlA MAMA NTILIE" imefeli kuonesha au kuwasilisha kazi yake ya fasihi kwa hadhira.
Amefeli kuonesha jinsi gani umaskini ni chanzo cha kutokuendelea kwa nchi. Mwandishi wa riwaya ameonesha thahiri kuwa katika riwaya hii kuna umaskini katika familia ya mzee lomolomo ila ameshindwa kuonesha ni kwa namna gani umaskini unapelekea nchi kutokuendelea.
Amefeli kuonesha athari za rushwa. Mwandishi wa riwaya hii ameonesha kuwa kulikua na rushwa katika kibanda cha mamantilie ambae alitoa rushwa kwa askari jiji ili aendelee kuuza katika jiji hilo. Mwandishi amefeli kuonesha ni kwa namna gani rushwa ni adui wa haki na hukota maendeleo hasi ya nchi.
Amefeli kuonesha suluhisho la ugomvi kati ya mzee lomolomo na familia yake. Mzee lomolomo alikua na mgogoro na familia yake na kwa hali hii ilipelekea yeye kutokuhudumia familia yake. Mwandishi ameshindwa kuonesha ni kwa namna gani Mgogoro huu ulifikia kikomo.


**Kielelezo Na. 10.2:** Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 10

Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejadili kushindwa kwa waandishi wa riwaya za "Watoto wa Mama N'tiliye" na "Takadini" badala ya kuchagua mhusika mmoja kwa kila riwaya na kuonesha namna walivyowasilisha mawazo matatu ya waandishi kwa kila kitabu kutoka katika riwaya mbili alizosoma.

### 2.3.1 Swali la 11: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi* hususani mada ndogo ya *Uhakiki wa Tamthiliya* na lililenga kupima umahiri wa mtahiniwa wa kuchambua na kutathmini maandishi ya kifasihi. Swali lilimtaka mtahiniwa kutumia tamthiliya mbili alizosoma kuonesha mikakati mitatu iliyotolewa na wasanii katika kupambana na changamoto zilizopo katika jamii.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 230,664 sawa na asilimia 43.57 ya waliofanya mtihani kwa kuwa lililkuwa la kuchagua. Swali lilikuwa na ufaulu wa mzuri sana ambapo watahiniwa 203,823 sawa na asilimia 88.36 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Hata hivyo, watahiniwa 26,841 sawa na asilimia 11.64 walikuwa na ufaulu hafifu. Chati Na. 9 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 11*

Chati Na. 9 inaonesha kuwa, watahiniwa 154,086 sawa na asilimia 66.80 walifaulu kwa kiwango kizuri cha alama 10 – 15; watahiniwa 49,737 (21.56%) walifaulu kwa kiwango cha wastani cha alama 4.5 – 9.5; na watahiniwa 26,841 (11.64%) walifaulu kwa kiwango hafifu cha alama 0 – 4.

Uchambuzi zaidi wa takwimu za ufaulu unaonesha kuwa watahiniwa 154,086 sawa na asilimia 66.80 ya waliofanya mtihani huu walikuwa na ufaulu wa juu kwa kupata alama kati ya 10 na 15. Miongoni mwao, asilimia 20.77 walikuwa na ufaulu wa juu kwa kupata alama 14 hadi 15 kutokana na watahiniwa hao kuonesha umahiri wa kutosha wa uhakiki wa kazi za fasihi andishi hususani uhakiki wa tamthiliya teule. Kutokana na umahiri huo, watahiniwa hao walifafanua kwa usahihi mikakati mitatu ya kupambana na changamoto zilizopo katika jamii kwa kila tamthiliya teule. Watahiniwa hao walionesha mikakati sahihi kama vile, *mapambano dhidi ya umasikini*, *UKIMWI* na *ulevi* kutoka katika tamthiliya ya "Orodha", mapambano dhidi ya *ulevi*, *imani potofu kuhusu sensa*, *ukiukaji wa taratibu za kufuatwa katika ndoa* (Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe) na mapambano dhidi ya *ndoa za utotoni*, *UKIMWI* na *mmomonyoko wa maadili* katika (Kilio Chetu). Watahiniwa hao walifafanua kwa usahihi namna wasanii walivyotumia mikakati hiyo kupambana na changamoto zilizopo katika jamii huku wakitoa mifano dhahiri kuthibitisha hoja hizo. Kielelezo Na. 11.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

1.1 Mikakati ni mbinu ambazo wasanii wana ziitumia ili kutafuta suluhisho la matatizo katika jamii yao. kwa kutumia tamthiliya ya "orodha" iliyo andikwa na "Steve Reynolds" na thamthiliya ya "kilio chetu" iliyo andikwa na "Medical Aid founda tion" mwandishi ana onyesha mikakati iliyotolewa na wasanii kama suluhisho la matatizo;

kwa kuanza na tamthiliya ya "kilio chetu" iliyo andikwa na "medical Aid foundation" mwandishi anaonyesha mikatati mbalimbali;

Mkakati wa kupiga vita mapenzi katika umri mdogo; Msanii amepiga vita mapenzi ya umri mdogo mapenzi hayo yalikua katika ya Joti na suzi walikua na mapenzi katika umri mdogo vika msababishia Joti kupata virusi vya ukimwi

Mkakati wa kutoa elimu ya jinsia kwa watoto na vijana; Msanii ~~anato~~ anaonyesha mkakati wake wa kuto elimu ya jinsia kwa vijana kama kina suzi, Joti wangepata elimu wasinge jiingiza katika mapenzi

Mkakati wa kutoa elimu juu ya njia za maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi; Mwandishi ~~ana~~ ame toa mkakati wa kuto elimu kwa jamii kwa njia za maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi Mfano Joti angepewa funzo kuhusu njia za kujikinga na ukimwi asinge pata ugonjwa huo.

kwa kumalizia na tamthiliya "orodha" iliyo andikwa na "Steve Reynold" mwandishi anaonye sha mikakati mbalimbali

11. Mkakati wa utoaji wa elimu juu ya njia
zakujikinga na ugonjwa wa ukimwi; ~~Mwandishi~~ huyu
alitaka kuto elimu kwa jamii kuonyesha njia
zakujikinga na ugonjwa wa ukimwi mwandishi
ametumia furaha angelipowa elimu juu ya janga
la ugonjwa wa ukimwi angejikinga nao.
Kupiga vita umaskini; umasikini ni tatizo
katika jamii yetu kama furaha alitamani ape
ndonge kama wasichana wengine laki hakuwa
na mbinu nyingine zaidi ya kutoroka na kwenda
kunywa pombe ili apate pesa za kununua nguo.
Mkakati wa kuwa na upendo katika jamii;
Mama furaha alionyesha upendo mkubwa kwa
Mwanae na kumhudumia alipukua na ugonjwa
pia furaha alionyesha upendo kwa jamii yake
kwa kuwaandikia orodha ya vitu vinavyo sababisha
maambukizi ya ugonjwa huo wa ukimwi
Hitimisho; ili kuondoa changamoto mbalimbali
lazima mtu awena mikakati ya kuondoa chang
amoto hiyo inayo wa sumbua katika jamii
yao.

**Kielelezo Na. 11.1:** Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 11


Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyebainisha kwa usahihi mikakati mitatu kutoka katika tamthiliya ya "Orodha" na "Kilio Chetu" iliyotolewa na wasanii ili kupambana na changamoto mbalimbali katika jamii.

Aidha, watahiniwa 49,737 sawa na asilimia 21.56 ya waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu wa wastani na kupata alama kati ya 4.5 na 9.5. Ufaulu huu ulitokana na watahiniwa hao kutokuwa na umahiri wa kutosha katika uchambuzi wa kazi za kifasihi, hivyo kuonesha baadhi ya mikakati iliyotolewa na wasanii ili kupambana na changamoto mbalimbali katika jamii na kushindwa kuonesha mikakati mingine kutoka katika tamthiliya teule. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha kwa usahihi mikakati

mitatu kutoka katika tamthiliya ya Orodha kama vile *mapambano dhidi ya umasikini*, *UKIMWI* na *ulevi* lakini hakuweza kubainisha mikakati hiyo katika tamthiliya ya Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe iliyohusu *mapambano dhidi ya ulevi*, *imani potofu kuhusu sensa*, *ukiukaji wa taratibu za kufuatwa katika ndoa;* hivyo kupata alama za wastani.

Vilevile, watahiniwa 26,841 sawa na asilimia 11.64 ya waliofanya mtihani walijibu vibaya swali hili na kuwa na ufaulu wa kiwango hafifu kwa kupata alama kati ya 0 na 4. Hali hii ilitokana na kukosa umahiri wa kutosha wa uhakiki wa tamthiliya teule, hivyo kushindwa kuonesha mikakati mitatu ya wasanii katika kupambana na changamoto katika jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijadili nafasi ya mwanamke katika jamii kuwa amechorwa kama *Chombo cha starehe*, *Mtu asiye na haki*, *Chombo cha kuburudisha watu*, *mlezi*, na *mzazi* kinyume na matakwa ya swali.

Watahiniwa wengine walibainisha migogoro mbalimbali iliyojitokeza katika tamthiliya teule bila kuhusisha na mikakati bayana ya kupambana na migogoro hiyo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alionesha mgogoro kati ya Suzi na mama yake baada ya Suzi kujiingiza kwenye mapenzi angali mwanafunzi katika tamthiliya ya "Kilio Chetu" lakini hakuonesha mikakati iliyotolewa na wasanii ili kuondokana na migogoro hiyo katika jamii. Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuonesha mikakati mitatu iliyotolewa na wasanii ili kupambana na changamoto mbalimbali katika jamii kupitia tamthiliya teule.


11 Mgogoro kati ya padri james na wanajamii wake;
mgogoro huu ulitokea pale ambapo padri James alikua
anategemewa katika mambo ya mungu na wanajam
ii afu yeye kuamua kutembea na furaha mtoto mdogo
ambaye alikua malaya wa hapo kijijini kwao hivyo padri
James watu walichukia kitendo hicho cha padri james na furaha.
Mgogoro kati ya furaha na mama yake; mgogoro huu
ulitokea pale ambapo furaha alikua anatembea na
padri james afu mama furaha alikua anamkanya -
furaha aache na tabia hiyo. kwa kuendelea na kitabu
kingine ambacho ni "ngoswe penzi kitovu cha uzembe" kilicho
andikwa na "E. Semzaba" Nitaelezea kama ifuatavyo.
Mgogoro kati ya ngoswe na mzee ~~na~~ mitomingi; -
Mgogoro huu umetokea pale ambapo ngoswe alikua amekuja -
kufanya zoezi la kuhesabu watu alafu yeye akawa ~~na~~ ame
acha zoezi hilo na kuanza kumtongoza mazoea na mwishowe takimu kuungua
Mgogoro kati ya mzee mitomingi na wakeze; mgogoro
huu umetokea pale ambapo mazoea alipotaka kutoroshw
a na ngoswe na mzee mitomingi akadhani kuwa wakeze wa
li walikua na taarifa hiyo ya mazoea kutoroshwa na ngoswe
kumbe walikua hawajui mzee mitomingi akawa na -
hofu kuwa ~~wakezang~~ wakeze wanajua suala hili halafu
hawakunijulisha.
Mgogoro kati ya ngoswe na jamii; mgogoro huu
umetokea pale ambapo ngoswe alipewa kazi ya kwenda
kuhesabu watu alafu yeye hakufanya hiyo alianza -
kufanya uzembe ~~e~~ wakutohesabu watu mpaka takri
mu zikaungua moto wanajamii na serikali ilichukia na -
kumlaumu ngoswe kwakufanya uzembe wakurudisha maendeleo nyuma
Hivyo basi; tunashauriwa kuwa makini katika
kufanya mambo yetu kwa ufasaha zaidi ili tusirudi
she maendeleo nyuma kama ngoswe alivyofanya.

**Kielelezo Na. 11.2:** Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 11

Kielelezo Na. 11.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyebainisha migogoro iliyojitokeza katika tamthiliya za “Orodha” na “Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe” badala ya kuonesha mikakati mitatu iliyotolewa na wasanii kwa kila kitabu kutoka katika tamthiliya mbili alizosoma, hivyo kupata 0.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KATIKA MADA

Mtihani wa somo la Kiswahili ulikuwa na maswali 11 yaliyotahiniwa kutoka mada sita (6) ambazo ni *Ufahamu*, *Matumizi ya Sarufi*, *Utumizi wa Lugha*, *Uandishi*, *Maendeleo ya Kiswahili* na *Fasihi*. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mada mbalimbali unaonesha kuwa, watahiniwa walifaulu katika mada zote zilizotahiniwa mwaka 2023 ambapo mada 4 zilikuwa na ufaulu wa kiwango kizuri na mada 3 zilikuwa na kiwango cha wastani. Kiwango kizuri zaidi kilikuwa katika mada ya *Ufahamu* (89.62%) iliyotahiniwa katika swali la 8 na kufuatiwa na mada za *Uandishi* (86.88%) katika swali la 7; *Fasihi* (72.87%) katika swali la 9, 10 na 11; na *Mada mchanganyiko* (64.76%) ilizotahiniwa katika swali la 1. Aidha, mada zilizokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu zilihusisha *Sarufi* (61.11%) katika swali la 3 na 4; *Maendeleo ya Kiswahili* (53.09%) katika swali la la 6; na *Utumizi wa Lugha* (38.61%) katika swali la 2 na la 5.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mada mbalimbali kwa mwaka 2023 unaonesha kuwa mada tano (5) kati ya sita (6) zilizotahiniwa ziliongezeka ufaulu ikilinganishwa na mwaka 2022. Kiwango cha ufaulu kiliongezeka kwa kiasi kikubwa katika mada ya *Uandishi* kutoka asilimia 35.65 hadi 86.88 ikifuatiwa na mada za *Sarufi* kutoka (37.35%) hadi (61.11%), *Fasihi* kutoka (60.78%) hadi (72.87%), *Maendeleo ya Kiswahili* kutoka (46.24%) hadi (53.09%) na *Ufahamu* kutoka (87.64%) hadi (89.62%) sawa na ongezeko la jumla ya asilimia 51.23, 23.76, 12.09, 6.85 na 1.98 mtawalia. Ufaulu huu unaonesha kuwa katika mtihani huu, watahiniwa wengi walikuwa na umahiri wa kutosha wa mada mbalimbali zilizotahiniwa kwani zaidi ya nusu ya watahiniwa walikuwa na ufaulu wa wastani hadi mzuri katika maswali mengi. Aidha, mada ya *Ufahamu* imeendelea kuimarika kwani ufaulu wake ulipanda kwa mfululizo kwa miaka minne (4) kuanzia mwaka 2020 hadi 2023 ambapo kiwango cha ufaulu kilikuwa asilimia 43.3, 75.68, 87.64, na 89.62 mtawalia.

Hata hivyo, ufaulu wa watahiniwa ulishuka katika *Mada Mchanganyiko* iliyokuwa na upungufu wa asilimia 18.65 kutoka asilimia 83.43 hadi 64.76.

Wastani wa ufaulu wa watahiniwa katika mada zote kwa mwaka 2023 ni asilimia 66.71. Kiwango hiki ni cha juu kwa asilimia 8.19 ikilinganishwa na mwaka 2022, ambapo wastani wa ufaulu wa mada ulikuwa asilimia 58.52.

Kwa upande mwingine, kiwango cha wastani cha ufaulu katika mada za *Utumizi wa Lugha* (38.61%), *Maendeleo ya Kiswahili* (53.09%) na *Sarufi* (61.11%) kilitokana na baadhi ya watahiniwa kukosa umahiri wa kutosha katika mada hizo. Watahiniwa hao walishindwa kubaini visawe na kuelezea maana za msingi na za ziada za maneno ya Kiswahili katika mada ya *Utumizi wa Lugha*; kuelezea mfanano uliopo kati ya lugha za Kibantu na Kiswahili (*Maendeleo ya Kiswahili*); na kushindwa kubaini njeo na nyakati mbalimbali pamoja na kuelezea dhima za uambishaji katika vitenzi vya Kiswahili (*Sarufi*). Ufaulu wa wastani wa watahiniwa katika mada hizo ni kielelezo kuwa jitihada zaidi zinahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji ili kuwapa wanafunzi umahiri wa kutosha. Ufaulu wa watahiniwa katika mada mbalimbali kwa mwaka 2023 umeoneshwa katika **Kiambatisho Pekee**.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, Mtihani wa somo la Kiswahili wa mwaka 2023 ulizingatia muhtasari wa somo la Kiswahili na maswali yote yalihusisha ngazi zote za utambuzi yaani *kukumbuka, kuelewa, kutumia, kuchambua, kutathmini,* na *kuunda*. Kiwango cha ufaulu kilikuwa kizuri ambapo asilimia 96.80 ya watahiniwa walifaulu.

Uchambuzi huu umebaini changamoto mbalimbali zilizosababisha ufaulu wa wastani katika mada za *Utumizi wa Lugha, Maendeleo ya Kiswahili,* na *Sarufi.* Sababu hizo zinahusisha kutozingatiwa ipasavyo kwa maelekezo ya maswali na uelewa mdogo wa baadhi ya mada zilizotahiniwa. Ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa mada zote katika mitihani ijayo, mikakati mbalimbali inahitajika katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mikakati hiyo ni muhimu hasa ikizingatiwa kuwa kwa sasa lugha ya Kiswahili ina hadhi kubwa kitaifa na kimataifa.

Vilevile, uchambuzi huu unaonesha kuwa, maswali yaliyohitaji umahiri wa juu wa kufikiri yalikuwa na kiwango cha chini cha ufaulu. Maswali hayo yalihusu mada za *Utumizi wa Lugha, Maendeleo ya Kiswahili*, *Sarufi* na *Uhakiki wa Ushairi* (Fasihi) ambazo zinahitaji mageuzi makubwa ya mbinu za ufundishaji ili ziwe na ufaulu mzuri wakati ujao. Miongoni mwake, mada ya *Utumizi wa Lugha* (38.61%) ilikuwa na ufaulu wa chini zaidi kwa mwaka 2023.

Mwisho, inatarajiwa kuwa taarifa hii itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika somo la Kiswahili na kutatua changamoto kwa walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali. Pia, taarifa hii

itawafanya walimu na wanafunzi kuyaelewa makosa mbalimbali yanayofanya ufaulu kuwa wa kiwango cha wastani au hafifu, hivyo kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kuinua kiwango cha ufaulu siku zijazo.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu katika mada za *Utumizi wa Lugha*, *Maendeleo ya Kiswahili*, *Sarufi* na *Uhakiki wa Ushairi* hususani kipengele cha *matumizi ya lugha* kutoka ufaulu wa wastani kuwa ufaulu mzuri inashauriwa kuwa:

(a) Mwalimu awaongoze wanafunzi kwa maswali, majibu na majadiliano ili kufafanua dhima ya uambishaji katika vitenzi vya Kiswahili.

(b) Wanafunzi wajadili katika vikundi njeo na nyakati mbalimbali zinazodhihirika katika vitenzi vya Kiswahili.

(c) Kwa kutumia onesho mbinu na chati ya tungo, mwalimu awaongoze wanafunzi kubaini visawe vya maneno mbalimbali ya Kiswahili. Pia, wanafunzi waongozwe kutunga sentensi kulingana na maana stahiki za visawe husika.

(d) Kwa njia ya utafiti, mwalimu awaongoze wanafunzi kufanyia utafiti lugha mbalimbali za Kibantu ili kubaini mfanano uliopo kati ya lugha hizo na lugha ya Kiswahili.

(e) Kwa njia ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kuelezea jinsi Kiswahili kinavyofanana na lugha za Kibantu kimsamiati na kimuundo.

(f) Wanafunzi washiriki katika majadiliano ya ukindu ili kubaini vipengele anuwai vya lugha katika diwani teule na kufafanua dhima zake katika kazi za kifasihi.

**KIAMBATISHO PEKEE: UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MWAKA 2023**

<table>
<tr><th rowspan="2">Na.</th><th rowspan="2">Mada</th><th colspan="2">Ufaulu kwa kila Swali</th><th rowspan="2">Wastani wa Ufaulu (%)</th><th rowspan="2">Maoni</th></tr>
<tr><th>Namba</th><th>% ya Ufaulu (alama 30⁺)</th></tr>
<tr><td>1.</td><td>Ufahamu</td><td>8</td><td>89.62</td><td>89.62</td><td>Vizuri</td></tr>
<tr><td>2.</td><td>Uandishi</td><td>7</td><td>86.88</td><td>86.88</td><td>Wastani</td></tr>
<tr><td rowspan="3">3.</td><td rowspan="3">Fasihi</td><td>9</td><td>42.03</td><td rowspan="3">72.87</td><td rowspan="3">Wastani</td></tr>
<tr><td>10</td><td>88.27</td></tr>
<tr><td>11</td><td>88.36</td></tr>
<tr><td>4.</td><td>Sarufi, Utumizi wa Lugha, Uandishi na Fasihi kwa Ujumla (Swali la Kuchagua)</td><td>1</td><td>64.76</td><td>64.78</td><td>Vizuri</td></tr>
<tr><td rowspan="2">5.</td><td rowspan="2">Sarufi</td><td>3</td><td>58.40</td><td rowspan="2">61.11</td><td rowspan="2">Wastani</td></tr>
<tr><td>4</td><td>63.80</td></tr>
<tr><td>6.</td><td>Maendeleo ya Kiswahili</td><td>6</td><td>53.09</td><td>53.09</td><td>Wastani</td></tr>
<tr><td rowspan="2">7.</td><td rowspan="2">Utumizi wa Lugha</td><td>2</td><td>49.85</td><td rowspan="2">38.61</td><td rowspan="2">Wastani</td></tr>
<tr><td>5</td><td>27.36</td></tr>
</table>